# Uamuzi wa Kimbingu

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mauʻudi na Imam Mahdi

# Uamuzi wa Kimbingu

Tafsiri ya Kiswahili ya: Asmani Faisala (Kiurdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri: Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1891
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2017

© Islam International Publications Ltd.


Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-555-2

# Jalada la chapa ya mara ya kwanza



هٰذا الذی کنتم بہ تستعجلون

(یہ وہی ہے جس کے لئے تم جلدی کرتے تھے)

میاں نذیر حسین صاحب دہلوی اور اُن کے شاگرد بٹالوی کو جو مؤلف رسالہ ہذا صاحب کتاب ازالہ اوہام و توضیح مرام
کو کافر اور دجال اور کذاب اور ملحد اور بے ایمان اور ملعون اور دور از رحمت رحمٰن ٹھہراتے ہیں اور
ایسا ہی اُن کے تمام ہم خیالوں مولویوں صوفیوں پیرزادوں فقیروں سجادہ نشینوں
کو آسمانی فیصلہ کی طرف دعوت اور نیز اُنکے گذشتہ مباحثات کی کیفیت

والحمد للہ والمنۃ کہ یہ رسالہ مسمّٰی

آسمانی فیصلہ

مطبع ہند ریاض امرتسر میں چھپا

ایک ہزار جلد فی سبیل اللہ تقسیم کی گئی ہے

# Jalada la chapa ya kwanza

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ وَالَّذِيْنَ مَعَهٗۤ اَشِدَّآءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ

جَآءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ اِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوْقًا

Haki imefika na batili imetoweka, na batili ndiyo yenye kutoweka.Muhammad ni Mtume wa Mungu na walio pamoja naye ni imara mbele ya makafiri, na ni wenye kuhurumiana wao kwa wao.

هٰذَا الَّذِیْ كُنْتُمْ بِهٖ تَسْتَعْجِلُوْنَ

Haya ndiyo mliyokuwa mkiyaharakia

Mwito kwenye Uamuzi wa Kimbingu kwa Bwana Mian Nadhir Husain na mwanafunzi wake Batalawii ambao wanamtaja mwandishi wa kijitabu hiki na mwandishi wa kitabu cha Izala Auhaam na Taudhihe Maraam kuwa kafiri, dajjal, mwongo, na mpotevu, asiye na imani, maluuni, mbali na rehema ya Rahmani, na kadhalika kwa wote wenye mawazo kama yao, masheikhe, masufii, mapirzada, madaruweshi na masajjada-nashin. Na pia imo humu hali ya mijadala yao ya zamani. Na sifa zote njema na shukrani ni ya Mungu kwamba kijitabu hiki kiitwacho.

# Uamuzi wa Kimbingu

Kilichapishwa katika matbaa ya Riadh Hind, Amritsar.

Nakala elfu moja zimegawiwa katika njia ya Mwenyezi Mungu

يٰحَسْرَةً عَلَى الْعِبَادِ مَا يَأْتِيْهِمْ مِّنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ

فَقَدْ كَذَّبُوْا بِالْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ فَسَوْفَ يَأْتِيْهِمْ اَنْبٰٓؤُا مَا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ

Na wameikadhibisha haki ilipowafikia, kwa hiyo hivi karibuni zitawafikia habari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

Ni sikitiko kwa watumishi: hakuwafikia Mtume yeyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha.

## Maelezo ya Mwenezi

Uamuzi wa Kimbingu ni tafisri ya kitabu Asmani Faisala kilichoandikwa na Seyidna Ahmad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, kwa lugha ya Kiurdu. Kitabu hiki kinafafanua baadhi ya mambo yaliyojiri baina ya Seyidna Ahmad a.s. na wapinzani wake masheikh fulani. Kwa vile maelezo yake ni ya kuvutia sana, basi Dawati la Kiswahili liliamua kutoa tafsiri yake kwa Kiswahili ili wanufaike kielimu wajuao lugha hii tukufu.

Kwa hisani yake, Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya alichukua jukumu la kukifasiri. Muswada ulipitiwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania. Kabla tafisri haijapelekwa mtamboni miye nalidurusu nikilinganisha na matini ya Kiurdu na kurekebisha palipostahili kurekebishwa.

Aidha, Sheikh Ansar Hussain na Sheikh Nasr Ahmad Bhatti walisaidia kupanga ibara zake kwa kompyuta, na Seyid Tanwir Mujtaba akatekeleza kazi ya *fometi*. Mwenyezi Mungu Awapatie hao wote malipo bora

sana hapa na huko Akhera.

Mwenyezi Mungu Awajalie wasomaji kunufaika na tafsiri hii kielimu.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah. Pakistan
19.03.2017

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [2]

لَنْ يَّجْعَلَ اللهُ لِلْكٰفِرِيْنَ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ سَبِيْلًا

Haiwi kuwa Mungu Awajaalie makafiri njia ya kuwalaumu waaminio.

اے خداوند رہنمائے جہان — آتش افتاد درجہان ز فساد
صادقاں را زِ کاذبانِ بُرہان — الغیاث اے مغیث عالمیان[3]

Uhakika hasa wa Sheikh Nadhir Husain kunikufurisha na hali ya kweli ya ushindi wake wa bandia, na mwito kwake na kwa wale wenye fikara kama zake kwenye uamuzi wa kimbingu.

Ingawa Sheikh Nadhir Husain wa Delhi mwenyewe pia hakuepukana na fatuwa za kukufurishwa, bali ndiye aliyetajwa kuwa kafiri wa kwanza katika India, hata hivyo yeye ana jazba kubwa ya kuwakufurisha Waislamu wengine jinsi watu wakweli wanavyokuwa

---

1 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Mwenezi.

2 Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu. Mwenezi.

3 Tafsiri ya beti za Kiajemi: "Ee Mola, Kiongozi wa ulimwengu, moto umeibuka ulimwenguni kwa sababu ya ufisadi. Wakweli wanayo hoja dhidi ya waongo. Ee Mfariji, tuondolee huzuni." Mwenezi.

na shauku ya kuwasilimisha watu. Yeye anaonekana kupenda sana jambo hili kwamba Mwislamu yeyote atolewe fatuwa ya kukufurishwa bila haki yoyote, hata kama sababu ya kukufurishwa isipatikane hata moja. Na mwanafunzi wake hodari Mian Muhammad Husain Batalawii anayeitwa shiekh, naye pia amefuata nyayo zake, bali bwana sheikh huyu amemzidi hata mwalimu wake katika harara na shauku ya kukufurisha. Inaonekana kuwa imani ya wote wawili, mwalimu na mwanafunzi, ni kwamba kama zinapatikana alama tisini na tisa wazi wazi za imani ya mtu sawa na mtazamo wao, na alama moja tu ya imani isipoeleweka kwao kutokana na upungufu wa kuelewa kwao, basi hata hivyo mtu huyo anafaa kuitwa kafiri. Na ndivyo jamaa hawa walivyonitendea hata mimi pia. Mtu asomaye kwa makini vitabu vyangu Barahine Ahmadiyya na Surma Chashme Aria, itabainika kwake jinsi mimi mnyenyekevu nilivyo hadimu wa dini ya Islam kwa kujitolea na kadiri ninavyojitolea kueneza adhama za Mtume Mtukufu[saw]. Lakini hata hivyo, Sheikh Nadhir Husain na mwanafunzi wake Batalawii hawakuvumilia mpaka wakaniamulia kuwa kafiri. Hali ya Sheikh Nadhir Husain ni ya kusikitisha sana, maana katika uzee huu huku akichungulia kaburini hakujali Akhera yake hata kidogo, na kwa kunitaja kuwa kafiri

aliachana kabisa na uaminifu na uchamungu. Hata baada ya kufikia ukingoni mwa mauti alionyesha mfano mbaya sana wa undani wake. Yafaa maulamaa wanyofu, washika dini na watawa wawajibike kutoharakia kumkufurisha mtu maadamu hawanazo mkononi mwao sababu sahihi, zenye yakini, za kweli kabisa, ambazo juu ya msingi wa kauli hizo mtu hulaumiwa kuwa kafiri, naye huyo mwenyewe akubali wazi wazi kwa mdomo wake kauli hizo zihakikishazo kufuru wala asizikatae. Lakini inatakiwa kuangalia kuwa je Sheikh Nadhir Husain ametumia njia hii ya ucha Mungu au amekanyaga pembeni kabisa? Hivyo basi, iwe wazi kuwa Sheikh Nadhir Husain ameiacha kabisa njia ya ucha Mungu na uaminifu. Mimi nilitoa vipeperushi vitatu katika Delhi na kueleza mara kwa mara katika vipeperushi hivyo kuwa mimi ni Mwislamu na itikadi zangu ni za Kiislamu, bali kwa kula kiapo cha Allah Mwenye shani adhimu nilifikisha ujumbe kwamba katika maandishi yangu au hotuba yangu yoyote hakuna jambo lolote ambalo, Mungu Apishe mbali, ni kinyume cha itikadi za Kiislamu. Ni kutoelewa tu kwa wapinzani wenyewe, waila kwa moyo wote ninaziamini itikadi zote za Islam na ninachukia itikadi zilizo kinyume na Islam. Lakini bwana Sheikh hakuzingatia kabisa maneno yangu na bila kufanya uchunguzi na utafiti wowote

yeye ameniita kafiri. Bali hata kwa kusikia kukiri kwangu mara nyingi

أَنَا مؤمن انا مؤمن[4], yeye akase لَسْتَ مُؤْمِنًا[5]. Na mara kwa mara katika maandishi na hotuba zake na katika vipeperushi vya wanafunzi wake ameniita kafiri, nisiye na dini, dajali, na kwa jumla akatangaza kuwa mtu huyu (yaani mimi) ni kafiri, hana imani na amejitenga na Mungu na Mtume[saw]. Hivyo, kutokana na kupuliza huku kwa Bwana Sheikh, dhoruba kali ikatokea ndani ya watu, na wakazi wa India na Panjab wakakumbwa na fitina kubwa, hususan wenyeji wa Delhi wakapamba moto kwa kuchochewa na kauli za bwana sheikh. Katika Delhi labda kuna Waislamu sitini au sabini elfu hivi, lakini Mungu ndiye Ajuaye zaidi kama mtu alikuwapo kati yao kwa nadra ambaye hakushiriki katika kunitukana, kunilaani na kunidhihaki au kuyasikia hayo. Akiba hiyo yote inahusikana na matendo ya Bwana Sheikh aliyojiweka katika siku za mwisho za uhai wake kwa ajili ya Akhera yake. Yeye kwa kuficha ushahidi wa kweli akaimarisha mioyoni mwa malaki ya watu kuwa mtu huyu (yaani mimi) kwa hakika ni kafiri, anastahili kulaaniwa na ametoka kutoka dini ya Uislamu. Nami siku hizo hizo nilipokuwa Delhi, kwa kuona kelele

4 Mimi na mwaminio, mimi ni mwaminio. Mwenezi.

5 Wewe si mwaminio. Mwenezi.

za kukufurisha zilizokuwa kote mjini, nikatoa kipeperishi maalum kumwambia huyo Bwana Sheikh na kumwandikia vilevile barua chache na kueleza kwa unyenyekevu kuwa mimi si kafiri, na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa mimi ni Mwislamu na ninaamini itikadi zote wanazoamini Ahlu-Sunnah wal-Jama'at na ninaamini Kalima Tayyiba لا إِلٰه الا الله محمد رسول الله. Ninasali sala kwa kuelekea kibla, mimi sidai unabii bali mwenye madai ya aina hii namwona kuwa ametoka kutoka ndani ya Uislamu. Niliandika pia kuwa mimi siwakatai malaika, wallahi mimi ninawaamini Malaika kama ilivyoaminiwa katika sheria. Nilieleza pia kuwa mimi siikatai Lailatul Qadri, bali naiamini ile Lailatul Qadri ambayo maelezo yake yameshatolewa ndani ya Kurani Tukufu na nikaeleza pia namwamini Jibril na wahyi wa utume, sikatai. Wala siikatai siku ya ufufuo na mkusanyiko, wala sishuku adhama kamili za Mola wangu na kudra zake kamilifu na ishara zaka kama wale wenye fahamu mbovu wanakana uwepo wa Mungu. Wala sikatai kuamini miujiza kwa sababu haieleweki akilini. Mara kadhaa nimeeleza ndani ya mikutano ya hadhara kuwa mimi nina yakini juu ya nguvu za Mwenyezi Mungu zisizo na mipaka, bali nionavyo mimi kudra isiyo na mipaka ni jambo la lazima la Uungu. Kama baada ya kumkubali Mungu

kisha isemwe kuwa Hawezi kufanya jambo fulani, basi Mungu wa namna hii siyo Mungu asilani. Mungu apishe mbali, kama Huyo ni dhaifu kiasi hicho, basi wale wamtegemeao wamejifia katika uhai wao na matumaini yao yote yamepotea bure. Bila shaka hakuna jambo lolote lisilowezekana Kwake. Naam, ni lazima jambo lile liwiane na shani na utukufu wa Mwenyezi Mungu, wala lisiwe kinyume cha sifa zake kamili na ahadi zake za kweli. Lakini juu ya ikrari zangu zote, Bwana Sheikh akaandika kwa uwazi kuwa umeishatolewa fatuwa ya kufururishwa, nasi tunakufahamu kuwa u kafiri, usiye na imani. Bali tarehe 20 Oktoba, 1891 iliyokuwa imepangwa kwa majadiliano, ambayo kabla ya tarehe hiyo matangazo yanayozungumzwa yalikuwa yameishatolewa tayari, Bwana Sheikh kwa kupiga chenga akatoa udhuru huu mara kwa mara kuwa wewe ni kafiri, thibitisha kwanza itikadi yako kuwa ni ya Kiislamu, ndipo ufanye majadiliano. Wakati huo pia, kwa adabu yote, ikasemwa kuwa mimi si kafiri, bali ninayaamini mambo yote ambayo Mwenyezi Mungu Ameyaweka kuwa itikadi za Waislamu. Bali kama lilivyoandikwa katika kipeperushi cha tarehe 23 Oktoba 1891, nikaandika maandishi kwa mkono wangu pia kwamba mimi naziamini itikadi hizi zote. Lakini ni masikitiko kwamba Bwana Sheikh huyo aliendelea

kunitambua kuwa kafiri na kuniandika kafiri na alikuwa na udhuru huu huu ambao kwa sababu yake hakujadiliana nami juu ya mada ya kifo na uhai wa Masihi a.s, kuwa eti huyu ni kafiri, vipi tujadilianaje na makafiri. Kama angekuwa na ucha Mungu hata kidogo ndani yake, basi toka wakati ule ule ambapo kipeperushi kilitolewa nami kushusiana na itikadi zote za Islam na mimi kuwa mwislamu, yeye angetengana na fatuwa ya kunikufurisha. Na kama alivyowatangazia maelfu ya watu fatuwa ya kunikufurisha, vivyo hivyo ndani ya mikutano ya hadhara kwa kukiri kosa lake angetoa ushahidi wazi wazi kuhusu Uislamu wangu na angejiepusha na dhana mbaya isiyo ya haki, angejitafutia udhuru mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kuondolea mbali madhara ya kueneza fatuwa ya kunikufurisha kinyume cha ukweli. Lakini yeye kamwe hakufanya hivyo, bali mimi nilipokuwa ningali mjini Delhi niliendelea kusikia hii tu kwamba Bwana Sheikh anatoa mdomoni mwake maneno machafu na mabaya dhidi yangu, na hakuacha kunikufurisha. Kwa njia zote juhudi zilifanywa ili aachane na mwendo huu mbovu na azuie ulimi wake, lakini alikwishazoea kusema kafiri, kafiri, kunihusu hata kwamba hakuweza kuuzuia ulimi wake. Na nafsi *Ammarah* ikautawala moyo wake kiasi hiki kwamba

haikubakia nafasi yoyote ya hofu ya Mwenyezi Mungu. فاعتبروا يا اولى الابصار[6] Mimi sasa sitaki kurefusha kunikufurisha kwake, kila mmoja ataulizwa juu ya kauli na matendo yake. Amali zake ni juu yake na amali zangu ni juu yangu. Lakini jambo la kusikitisha ni hili kuwa yeye alizingatia tuhuma zisizo za haki na mambo ya uzushi tu, na jambo la asili lililostahili kujadiliwa na kubishaniwa yaani kifo cha Masihi[as] hakuligusia hilo hata kidogo. Nilimwandikia mara kadhaa kuwa mimi si mpinzani wako katika itikadi nyingine yoyote ila tu ninakupinga katika jambo hili kuwa siamini kama wewe uhai wa kimwili wa Hadhrat Masihi[as]. Bali ninamtambua Hadhrat Masihi[as] kwa imani na yakini kwamba ameishakufa na ameshajiunga na wafu, na nina yakini juu ya kifo chake. Na kwa nini nisikiamini kifo chake ambapo Mola wangu, Bwana wangu, ndani ya Kitabu chake Kitukufu, Kurani Tukufu, amemjumuisha katika kundi la wafu. Na ndani ya Kurani Tukufu nzima hakuna mahali popote panapoonyesha uhai wake kinyume na desturi wala kurejea kwake tena duniani, bali baada ya kueleza tu kifo chake ikanyamaza. Hivyo, kuwa kwake hai na pamoja na mwili wake huu huu na kisha kuja tena duniani wakati fulani naliona hili kuwa ni kinyume cha si tu ufunuo wangu, bali

---

6 Basi jifunzeni somo, enyi wenye busara. Mwenezi.

naifahamu fikara hii ya uhai wa Masihi[as] kuwa ni upuuzi na batili sawa na aya za wazi na za yakini kabisa za Kurani Tukufu. Kama kauli yangu hii ni kufuru au ni uongo, njoo basi, ukajadiliane nami juu ya jambo hili. Na kama ukithibitisha kutoka ndani ya Kurani Tukufu au ndani ya hadithi za Mtume[saw] uhai wa kimwili wa Hadhrat Isa[as], basi mimi nitajirudi kwa kauli yangu hii, bali nitachoma vitabu vyangu nilimoandika habari hizi. Kama huwezi kujadiliana, njoo basi, ule kiapo juu ya mada hii kwamba ndani ya Kurani Tukufu hamna habari inayozungumzia kifo cha Masihi, bali mna maelezo juu ya uhai wake, au ipo hadithi sahihi *marfuu muttasil*[7] ya Mtume[saw] ambayo kwa kutoa maelezo tofauti ya neno *TAWAFFI* imetoa ushahidi juu ya uzima wa kimwili wa Masihi. Kisha mpaka kwa muda wa mwaka mmoja kama ishara yoyote iliyo wazi haidhihiriki kuwa wewe ulikula kiapo cha uongo, yaani wewe usipopatikana na janga lolote kubwa, mimi bila kuchelewa nitatubu kwa mkono wako. Ni masikitiko kwamba Bwana Sheikh akaombwa mara kwa mara, lakini hakufanya mjadala wala hakula kiapo wala hakuacha kuniita

[7] Marfuu Muttasil ni Hadith ambayo mnyororo wa wasimulizi wake unamfikia Mtume Muhammad[saw] na ambayo wasimulizi wake wote wanapatikana mfululizo hadi Mtume Muhammad[saw]. Mwenezi.

kafiri, kafiri. Lakini kwa kuficha kutoka watu lawama za kuhepa kwake alitoa vipeperushi vya uongo ambamo iliandikwa mara kwa mara kwamba yeye aliendelea kuniita kujadiliana mpaka mwisho na alikuwa tayari pia kula kiapo, lakini eti mimi nilimwogopa yeye na sikuja kukabiliana naye. Kujiita Sheikh na Sheikh wa kote pote na kuongopa kiasi hiki! Mimi nisemeje juu yake على الكاذبين[8], Mwenyezi Mungu Amrehemu. Enyi wasomaji! Kama mna nuru ya busara, fahamuni kwa yakini kwamba mambo haya yote ya Bwana Sheikh na wanafunzi wake ni uongo mtupu, na ni porojo potovu. Kwa hakika mimi nilifululiza kutoa matangazo kwamba Bwana Sheikh afanye mjadala na mimi kuhusu kifo cha Masihi[as], na kwa kusudio hili hili nilijikalifisha na kukaa Delhi kwa kutumia gharama kwa mwezi mzima. Hivyo basi kila mtu mwenye busara anaweza kufahamu kuwa kama Bwana Sheikh angekuwa tayari kwa moyo mkunjufu kwa ajili ya mjadala, kwa nini mimi nisingejadiliana naye! Kuna msemo maarufu kuwa ukweli hushinda. Mimi niko tayari tena kujadiliana juu ya kifo cha Masihi kama nilivyokuwa tayari hapo awali. Bwana Sheikh akikubali kuja Lahore kufanya mjadala, mimi mwenyewe nitamgharamia nauli yake binafsi ya kwenda na kurudi. Kama yuko radhi kuja,

**8** ...(Laana) iwe juu ya waongo. Mwenezi.

hapo yeye akiniandikia ninaweza kumtumia nauli mapema bila kuchelewa. Mimi sasa sitaki kwenda Delhi, kwani nimekwisha ziona kelele na vurugu za wakazi wa Delhi na nimeisha sikia maneno yao ya shari wanayopayukapayuka [9] وَلَا يُلْدَغُ الْمُؤْمِنُ مِنْ جُحْرٍ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ. Mimi ninasema pia kuwa kama nikiepa kufanya mjadala juu ya kifo cha Masihi[as] kwa mujibu wa [10] صدّعن سبيل الله laana elfu moja za Mwenyezi Mungu ziwe juu yangu. Na kama sheikh wa kote pote auepe (mjadala), basi hata nusu yake ziwe juu yake. Na kama anasita kuja, mimi ninampatia hii ruhusa pia kwamba yeye afanye mjadala kupitia maandishi kwa kudhihirisha haki akiwa mahali pake tu. Ilmuradi, mimi nipo tu kwa kila hali na ninasubiri jibu murua kutoka kwa Bwana Sheikh. Mimi ninamwelekea kwa hamu Bwana Sheikh kwa sababu watu wanamdhania kuwa yeye ndiye anawashinda wote katika elimu na ni kama mzizi kati ya maulamaa wa Bara Hindi. Na hakuna shaka kwamba kwa kukata mzizi matawi yote yataanguka yenyewe. Ndiyo maana inanipasa kukazania mzizi tu, matawi yatajiishia yenyewe. Na kwa mjadala huu dunia itadhihirishiwa kuwa Sheikh wa kote kote ana hoja gani za yakini juu ya uhai wa kimwili wa Masihi[as] ambazo kwa sababu yake

**9** Mwaminio haumwi mara mbili katika shimo moja. Mwenezi.
**10** Kuwazuilia (watu) njia ya Mungu. Mwenezi.

amechochea chuki na hasira ndani ya watu wa kawaida. Lakini ikumbukeni bishara hii pia kuwa yeye kamwe hatafanya mjadala, na kama akifanya basi atafedheheka kiasi kwamba hataweza kuonyesha uso wake popote pale. Hae, namsikitikia sana kuwa yeye ameficha ukweli kwa kupenda heshima ya maisha ya siku chache. Ameuacha ukweli na akapenda uongo. Yeye alikuwa akijua vizuri kuwa kifo cha Hadhrat Masih[as] kimethibitika vizuri na Kurani Tukufu na Hadithi sahihi *marfuu* lakini kwa hiana tupu na ujanja anahepa makusudi kutoa ushahidi. Akiwa adui kabisa wa ukweli akaeneza baina ya watu kwa kuongopa kuwa ndani ya Kurani Tukufu imeandikwa hii tu kwamba Masihi bin Maryamu amenyanyuliwa mbinguni akiwa hai na mwili wake na habari ya kifo chake haiko popote pale. Lakini, kwa vile alikuwa anajua moyoni kuwa yeye hayuko kwenye haki na anasema kinyume cha Kitabu cha Mungu, kwa hiyo hakuja kwa nia safi kukabiliana nami katika kufanya mjadala, na kwa masharti mabovu akakwepa njia hii fupi na safi ya mjadala kuhusu kifo. Jambo la kuchukiza ni hili kwamba Mwenyezi Mungu mwenye shani na jalali Aseme kuwa Masihi bin Mariamu amefariki na Sheikh Nadhiir Husain aseme la, hapana kabisa, bali alinyanyuliwa mbinguni akiwa hai na mwili wake. 'Shabashi'! Ewe Nadhiir Husain,

uliifuata vizuri Kurani Tukufu! Ajabu zaidi ni kwamba ndani ya Kurani Tukufu hakuna popote palipotajwa kunyanyuliwa mbinguni, bali mmeelezwa kuinuliwa kwake baada ya kifo kama waambiwavyo wafu wote wakweli:[11] اِرْجِعِيْٓ اِلٰى رَبِّكِ . Basi, hiyo hiyo رفع الى الله[12] na[13] رجوع الى الله ambayo sharti lake ni kutokea kifo kwanza, ndiyo aliyopata Hadhrat Masihi pia. Wapi hii رفع الى الله na wapi hii رفع الى السماء ?? Hae, ni jambo la kusikitisha jinsi watu hawa walivyoitupa Kurani Tukufu kisogoni na jinsi utukufu wa Kurani Tukufu mara moja ukaondoka mioyoni mwao, na badala ya Neno Takatifu la Mungu wakaanza kuipenda desturi isiyo na msingi. Hawa wanabeba lundo la vitabu, lakini Mwenyezi Mungu Amewaondolea ufahamu. Fikara ya ushindi na ushinde imeshinikiza imani na uaminifu. Kiburi na kujitukuza kumewatupa mbali na kuikubali haki. Mimi sihuzuniki hata kidogo kuwa Sheikh Nadhir Husain na wanafunzi wake wameueneza ushindi wa uongo kinyume cha ukweli na wameificha hakika yenyewe, wala hilo si jambo la kunihuzunisha hata kidogo. Kwani katika hali ambapo ukweli na jambo la haki ni hili tu kwamba Bwana Sheikh kwa kweli

---

**11** Rejea kwa Mola wako. Al- Fajr, 89:29. Mwenezi.
**12** Kunyanyuliwa kwa Mungu. Mwenezi.
**13** Kurejea kwa Mungu. Mwenezi.

amepata kushindwa kwa kudumu na kukimbia, naye ameanguka hata kwamba sasa hatainuka tena hadi aondoke duniani katika hali hii ya kushindwa. Na endapo kwa ajili ya kuficha lawama ya watu aweke mandhari ya ushindi wa bandia mbele ya macho yake na kwa dakika chache ajifurahishe, kwa nini mimi nione vibaya? Bali kama akiangaliwa kwa jicho la huruma, hii ni haki yake pia, kwani najua kwa yakini kuwa yeye baada ya kushindwa kabisa mikononi mwangu amevumilia huzuni na hasira nyingi sana, na katika umri huu wa mwishoni amepata pigo kubwa la aibu na soni moyoni. Sasa kwa kujifariji kama hangejitangazia ushindi kinyume cha ukweli, hapo vipi moyo dhaifu wa uzeeni ungeweza kuhimili pigo hili kubwa! Hivyo, labda kwa kuona ni faradhi kuhifadhi uhai wake akajihalilishia uongo mkubwa sana. Nami hata sasa sikuwa na haja ya kwamba mimi kwa kuonyesha hakika yenyewe ya habari nifutilie mbali furaha yake ya bandia, kwani kufikiria kushinda na kushindwa ni wazo lisilo la busara; na waupendao ukweli huupenda ukweli tu hata kama upatikane katika sura ya ushindi au kwa sura ya ushinde. Lakini kwa vile watu hudanganyika kutokana na maandishi yasiyo ya kweli kama hayo na yenye upinzani, nao kwa kuathirika na uenezaji kinyume na haki, huyachukulia maandishi hayo kuwa sahihi na yenye maana na kisha

athari zake mbaya huiharibu sana dini za watu, hivyo kwa kudhihirisha uhakika hasa kulikuwa ni haki ya lazima na deni iliyo wajibu juu yangu ambao usingeondolewa bila kutoa. Lakini ninasikitika kuwa katika hali ya uzee wa Sheikh huyo mimi nimekuwa sababu ya kumkumbusha huzuni yake mara nyingine tena.

Hapa inafaa kuelezea pia kuwa miongoni mwa dhuluma alizonifanyia Bwana Sheikh bila haki ni kumwachia uhuru Batalawii, na akaridhika kuwa aishambulie heshima yangu kwa kunitolea matusi ya kila aina na kunilaani. Basi baada ya kutambua utashi wa Bwana Sheikh, yeye akapita kiasi na asipoijali aya tukufu[14] لَا يُحِبُّ اللّٰهُ الْجَهْرَ بِالسُّوْٓءِ akaja kutoa matusi machafu yale yanayowashinda hata matopasi na watu duni kiasi kwamba huyu mwenye tabia 'safi' akanitolea matusi machafu mbele ya mamia ya watu ndani ya msikiti wa Ijumaa wa Delhi. Miongoni mwa walioyasikia ni msaidizi wangu Sheikh Haamid Ali pia aliyekuwepo wakati huo. Watu wengine nao wanasadikisha yote hayo pia. Vile vile bwana huyu hata kwenye stesheni ya Phalor mbele ya kundi la watu akasema kunihusu kuwa huyu atakufa kifo cha mbwa. Na katika maandishi ya kawaida akanipachika

14 Mungu Hapendi jambo baya lisemwe. An-Nisaa, 4:149. Mwenezi.

jina la kafiri na dajali. Na katika postikadi ya tarehe 11 Oktoba 1891 aliyomwandikia Munshi Fateh Muhammad mfanyakazi wa Utawala wa Jammu, iliyoko mbele yangu wakati huu, haikuandikwa chochote ndani yake ila ni matusi tu. Kutoa matusi machafu katika maandishi ya wazi na kutumia midomo michafu katika postikadi zinazoweza kusomwa na kila mtu na kufikisha jazba mbaya ya upinzani hadi mwisho, je, Mungu Anapenda tabia hii? au inaweza kuitwa mwendo wa waungwana? Ndani ya postikadi ya tarehe 11 Oktoba, mzee huyu kwa harara ya hali ya juu kabisa akaandika kunihusu mimi kwamba mtu huyu kwa kweli ni kafiri, dajali, hana dini na ni mwongo mkubwa. Ewe Mola wangu! Ee Bwana wangu Mpendwa! Mimi nimekuachia Wewe jibu la maneno yake makali, laana na matusi. Kama haya ndiyo matakwa yako basi na matakwa yangu ndiyo matakwa yako. Mimi sihitaji zaidi ya hii kwamba uniridhie. Moyo wangu haukufichika kwako, macho yako yananiona mpaka ndani mwangu. Kama ndani yangu kuna tofauti, naomba uiondoe. Na kama unaniona nina ubaya fulani, basi ninajikinga nao kwa Uso wako. Ewe Mwongozi wangu Mpendwa! Kama mimi nimechagua njia ya maangamio, basi niepushe nayo, na nijaalie nifanye kazi ambayo ndani yake mna ridhaa yako. Roho

yangu inanena kuwa Wewe U kwangu na Utabaki kuwa wangu. Tangu Uliponiambia kuwa Mimi niko pamoja nawe na tangu uliposema kuniambia [15] إِنِّي مُهِينٌ من اراداهانتك na tangu uliponieleza kwa kunipa moyo na kunituliza kuwa [16] انت منى بمنزلة لا يعلمها الخلق , basi papo hapo mwili wangu ukapata nguvu mpya, maneno yako yatulizayo moyo ni marhamu ya majeraha yangu, maneno yako ya upendo ndiyo yenye kuchangamsha moyo wangu ulioumia sana. Mimi nilikuwa nimezama katika huzuni, Wewe ukanipa bishara. Nilikuwa nimekumbwa na misiba, Wewe ukanifariji. Mpendwa wangu! Furaha hii inanitosha kuwa U kwangu, nami ni kwako. Mashambulizi yako yatavunjilia mbali safu za maadui, na ahadi zako zote takatifu zitatimia, Wewe Utakuwa Msamehevu kwa mtumishi wako.

Nikirejea tena kwenye madhumuni ya awali, nataka kuwabainishia wasomaji kuwa mimi kadri nilivyoandika lugha chafu ya Bwana Batalawii nimeieleza kwa mfano tu, waila matusi ya mtu huyu hayana kikomo chake. Kwa hakika matusi hayo ni ya Sheikh Nadhir Husain, kwani mwanafunzi kamwe hawezi kujasiri kinyume na matakwa ya mwalimu

**15** Nitamfedhehesha yule atakayetaka kukufedhehesha. Mwenezi.
**16** Wewe unatokana nami katika eneo lisilojulikana kwa viumbe (watu). Mwenezi.

wake. Bwana Sheikh mwenyewe pia akatukana na kutukanisha pia. Na Bwana Sheikh hakuona makuruhu ndani ya matusi mabaya ya bawana Batalawii. Na bwana Batalawii akiwa amekaa katika nyumba ya Bwana Sheikh akaandika tangazo lingine lililojaa kiburi, ambamo akaandika sentensi hii kunihusu mimi: "Huyu ni windo langu, kwa bahati yake mbaya amekuja tena Delhi mikononi mwangu, nami nina bahati nzuri kuwa nimempata tena windo aliyekuwa amekimbia." Enyi wasomaji! Hebu semeni kwa uadilifu ni ya aibu namna gani maneno hayo!! Nasema kweli kabisa kwamba wanaopata riziki kidogo kwa kuwachekesha watu na kina damisi wenye adabu wa zama hizi pia wanaona haya kidogo, na watu duni tangu vizazi hata vizazi pia hawasemi maneno ya kiburi yenye aibu na majisifu mbele ya aelewaye hali yao halisi. Mimi kama ningekuwa windo la bwana Batalawii, kwa nini basi ningeenda Delhi na kumkamata mwalimu wake? Je mwanafunzi ni mkubwa kuliko mwalimu? Wakati mwalimu mwenyewe alikamatwa nami mithili ya shorewanda, sasa wasomaji waelewe kuwa mimi ni windo la Batalawii, au Batalawii ndiye windo la windo langu? Ufedhuli wa bwana Batalawii umefikia kilele na ndani ya ubongo wake mna mdudu ambaye siku moja Mwenyezi Mungu

lazima Atamtoa. Ni masikitiko kuwa siku hizi maisha ya wapinzani wetu yanategemea uongo na masingizio tu, na wanataka kujenga heshima zao kwa kiburi cha aina ya ki-Firauni. Firauni mpaka siku alipoghariki pamoja na jeshi lake aliendelea kudhani kuwa Musa ni windo lake, lakini mwishoni mto *Nile* ndio ulionyesha kuwa nani hasa alikuwa windo. Mimi nasikitika kuwa mashindano ya mshindani asiyejimudu yamenilazimu kutumia maneno makali kiasi fulani, waila tabia yangu ya asili ni mbali na kutoa neno kali mdomoni. Sikutaka kusema chochote, lakini bwana Batalawii na mwalimu wake wakanifanya niseme. Hata sasa ni afadhali bwana Batalawii abadili mwenendo wake, ajizuie ulimi wake, la sivyo atazikumbuka siku hizi huku akilia وما علینا الا البلاغ المبین[17] بادرد کشاں ہر کہ در افتاد در افتاد

گندم از گندم بروید جو ز جو    از مکافات عمل غافل مشو[18]

Wale watu wanaofurahia matangazo hayo ya uongo yazungumziayo ushindi wa bandia wa Sheikh Nadhir Husain, mimi nawasihi kwa ajili ya Mungu tu kuwa katika kuongopa huku wasijichukulie dhambi pasipo

---

[17] Yeyote agombanaye na wakamilifu atapata kuangamia. Na siyo juu yetu ila kufikisha kwa uwazi. Mwenezi.

[18] Ngano huzalisha ngano, na shayiri, shayiri. Usighafilikie malipizi ya amali. Mwenezi.

sababu. Katika tangazo langu la tarehe 11 Oktoba 1891, mimi nilieleza kwa kirefu kuwa Bwana Sheikh ndiye aliyekwepa kufanya mjadala. Ni shari gani hii na masingizio yaliyoenezwa pasipo kuona haya dhidi yangu kuwa eti mimi nimemwogopa Sheikh Nadhir Husain, Mungu Apishe mbali. Mimi kamwe sikumwogopa, na kwa nini ningemwogopa? Kutokana na busara niliyopewa toka mbinguni, mimi ninawatambua masheikh hawa duni kuwa ni vipofu. Wallahi hawa siwalinganishi hata na mdudu aliyekufa. Je mtu aliye hai anawaogopa wafu? Fahamuni kwa yakini kuwa elimu ya dini ni siri za kimbingu, na yule tu anaijua siri ya kimbingu ipasavyo ambaye anapata fadhili kutoka mbingu. Amfikiaye Mwenyezi Mungu, ndiye azifikiaye siri za kina za Neno lake pia. Akaaye katika mwanga kamili, yeye ndiye huwa na busara kamili pia. Naam, kama ingesemwa kuwa mimi niliogopa matusi yake machafu na nikatishika kwa matamshi yake yaliyojaa najisi, hapo pengine ingekuwa kweli kidogo, kwani daima watu waungwana huwaogopa watu wenye lugha chafu, na watu waliostaarabika hujitenga na watu wenye midomo michafu. شریف از سفلہ نمے ترسد بلکہ از سفلگی او مے ترسد[19] Ukweli

[19] Mtu mwema hamwogopi mwovu bali huuogopa uovu wake.

halisi ni huu kuwa Mwenyezi Mungu Alikusudia Adhihirishe aibu za Sheikh Nadhir Husain na Awafichulie watu hakika ya dundo lake. Basi watu wenye busara wanafahamu kuwa utashi wa Mungu umetimia, na uhakika wa uchamungu wa Nadhir Husain na ibada yake na elimu na maarifa yake umejulikana wazi. Kwa kuacha Ucha Mungu ameshapata dhila moja. Lakini dhila nyingine bado imebaki ambayo iko tayari kwa ajili yake na kwa wanaoafikiana na fikara kama zake ambayo tunaieleza hapa chini:

اے خدا اے مالک ارض و سما　　اے پناہ حزب خود در ہر بلا
اے رحیم و دست گیر و رہنما　　ایکہ در دستِ تو فصل است و قضا
سخت شورے اوفتاد اندر زمین　　رحم کن برخلق اے جان آفرین
امر فیصل از جناب خود نما　　تا شود قطع نزاع و فتنہ ہا
اک کرشمہ اپنی قدرت کا دکھا　　تجھ کو سب قدرت ہے اے ربّ الوریٰ
حق پرستی کا مٹا جاتا ہے نام　　اک نشاں دکھلا کہ ہو حجت تمام[20]

---

Mwenezi.

[20] Ee Mungu, ee Mmiliki wa ardhi na mbingu,
Ee Mwenye kulinda kundi lako katika kila balaa.

Ee Mwingi wa rehema na Msaidizi na Mwongozi,
Ewe ambaye mkononi mwako mna uamuzi na hukumu.

Vurugu zimetapakaa sana ardhini,
Uwahurumie viumbe, Ee Mwumbaji.

الهام اللہ تعالیٰ[21]

Ufunuo wa Mwenyezi Mungu:

كِتَابٌ سَجَّلْنَا مِنْ عِنْدِنَا

Hiki ni kitabu ambacho tulikipigia muhuri kutoka kwetu

## Uamuzi wa Kimbingu

Kabla sijaelezea uamuzi wa kimbingu, yalazimu kuandika kiasi hiki kwa kutoa maelezo safi kuwa jambo hili ni dhahiri kwamba watu ambao kwa kweli ni waaminio mbele ya Mwenyezi Mungu na waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu hasa kwa ajili yake, na Amewatakasa kwa Mkono wake, na kuwapa nafasi katika kundi lake teule na kuwahusu Amesema:[22] فِيْ وُجُوْهِهِمْ مِّنْ اَثَرِالسُّجُوْدِ , lazima zipatikane alama za sijida na ibada katika hao. Kwani katika ahadi za Allah hakuna makosa wala kutotimiza, hivyo basi kupatikana kwa alama zote hizi ndani ya

---

Udhihirishe jambo la kutoa uamuzi kutoka kwako,
Ili mabishano na fitina ziishe.

Uonyeshe nguvu ya kudra yako,
Kwani, unao uwezo wote, Ee Mola wa viumbe.

Uchamungu upo karibu kufutika,
Onyeshe, basi, ishara moja ili hoja ikamilike. Mwenezi.

[21] Ufunuo wa Mwenezi Mungu:

[22] Alama zao ni katika nyuso zao kwa athari ya kusujudu. Al-Fat'h 8:30. Mwenezi.

mwaminio, ambazo zimeelezwa ndani ya Kurani Tukufu zikiwa sifa za waaminio, ni miongoni mwa mahitaji ya imani. Na alama hizo hizo ndizo kigezo na kipimo kamili cha kupambanua kati ya waaminio na mtu ambaye maulamaa wa kaumu yake waliamwita kafiri, mzushi, dajali, na asiye na dini. Hivyo basi, mtu akimtajia nduguye Mwislamu kuwa kafiri, na asiridhike kutoka kwake hata kama huyo anakiri kuwa yu mwenye imani, na anaiamini Kalima takatifu لَآ اِلٰه اِلَّا الله محمّد رسول الله na anaziamini itikadi zote za Uislamu, na anaamini faradhi, kanuni za adhabu, na maagizo yote ya Mwenyezi Mungu kuwa faradhi, kanuni za kuadhibu maagizo, na anayatekeleza sawa na uwezo wake. Basi, hatimaye, njia ya kufanya maamuzi ni hii kuwa makundi yote mawili yapimwe kwa alama ambazo Mwenyezi Mungu Amezieleza ndani ya Kurani Tukufu kwa kudhihirisha tofauti baina ya mwaminio na kafiri, ili yule mtu ambaye kwa kweli mbele ya Mwenyezi Mungu, ni mwaminio, Mwenyezi Mungu Amwondolee sawa na ahadi yake tuhuma ya ukafiri, na Abainishe tofauti kati yake na wengine, na hivyo umalizike kabisa mzozo wa kila siku. Jambo hili anaweza kulielewa kila mwenye akili, kuwa ikiwa mimi — wanavyonifikiria Sheikh Nadhir Husain na mwanafunzi wake Batalawii — kweli ni kafiri, dajali, mzushi, mlaaniwa na mwenye kutoka nje

ya Uislamu, basi wakati wa kukabiliana Mwenyezi Mungu hataonyesha ishara yoyote ya waaminio kwa kunisadikisha. Maana, Mwenyezi Mungu kamwe Hadhihirishi msaada wake kwa kuonyesha alama za imani, kuwahusu makafiri na wapinzani wa dini yake ambao hawana imani na wamekataliwa. Na kwa nini awasaidie ilhali anawajua kuwa hao ni maadui wa dini na hawana neema ya imani. Hivyo, basi, kama Sheikh Nadhir Husain na bwana Batalawii walivyotoa fatuwa dhidi yangu ya ukafiri na ukosefu wa dini, endapo mimi kwa kweli ni kafiri, dajali na adui wa dini, basi katika mapambano hayo Mwenyezi Mungu Hatanisaidia, bali Atanidhalilisha kwa kutokunisaidia jinsi mwongo mkubwa apasavyo kuadhibiwa. Katika hali hii, Waislamu watasalimika na shari yangu, na Waislamu wote watapata amani na fitina yangu. Lakini kama kwa maajabu ya kudura ya Mungu, Sheikh Nadhir Husain mwenyewe na watu wa kundi lake, bwana Batalawii na wengineo, wakikosa kupata ishara za kuwasaidia, na msaada wa Mungu ukiwa pamoja nami, basi katika hali hii pia ukweli utawadhihirikia watu na mizozo ya kila siku itafikia kikomo chake.

Sasa yapasa kufahamu ya kwamba Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu Amewatolea wacha Mungu na waaminio wakamilifu ahadi ya kujaliwa misaada

minne mikubwa sana ya kimbingu ambayo ndiyo alama kamili za utambulisho wa mwaminio kamili. Nazo ni hizi:

Mosi, mwaminio kamili mara nyingi hupokea bishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu, yaani yeye huambiwa habari njema kabla hazijatokea zinazohusu makusudio yake au matakwa ya marafiki zake.

Pili, mwaminio mkamilifu hufunuliwa mambo ya ghaibu siyo tu yanayomhusu yeye na jamaa zake, bali kudura ya Mungu itakayodhihiri duniani au mabadiliko yoyote yatakayotokea kwa baadhi ya watu mashuhuri duniani, mwaminio mteule mara nyingi hupewa habari zake.

Ya tatu, maombi mengi ya mwaminio mkamilifu hukubaliwa, naye mara nyingi huarifiwa pia mapema kabla ya wakati wake juu ya kupokelewa kwa maombi hayo.

Ya nne, mwaminio kamili hufunuliwa zaidi kuliko wote elimu ya ndani na maarifa mapya na mambo ya kina na elimu za ajabu za Kurani Tukufu.

Katika alama hizi nne mwaminio mkamilifu huwashinda wengine mara nyingi. Ingawaje hii siyo kanuni hasa kuwa mwaminio mkamilifu daima aendelee kupata bishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kila dua yake lazima ikubaliwe bila

kukataliwa, na siyo lazima pia kuwa aarifiwe kila tukio litukialo duniani na kwamba maarifa ya Kurani Tukufu yaendelee kufunuliwa kwake, lakini wakati wa kushindana na watu wengine, alama hizi nne kwa wingi hupatikana kwa mwaminio mkamilifu tu. Ingawa inawezekana pia kuwa mtu ghairi yake, kwa mfano mwaminio asiye kamili, kwa nadra apewe sehemu fulani ya neema hizi, lakini mrithi wa kweli wa neema hizi ni mwaminio kamili tu. Naam, ni kweli kuwa daraja hii kamili ya mwaminio haiwezi kudhihirika bila mashindano kwa kila goigoi mwenye mtazamo finyu. Kwa hiyo, njia iliyo wazi na nyepesi ya kumtambua mwaminio wa kweli na kamili ni kufanya mashindano tu. Kwani, ingawa ishara hizi zote hudhihirika zenyewe pia kwa mwaminio mkamilifu, hata hivyo kuna vikwazo pia kama hakuna mashindano. Kwa mfano, pengine mwaminio kamili hufikiwa na watu wale pia watakao kuombewa ambao katika bahati yao hakuna kabisa kupata ufaulu na uamuzi wa Mungu kwa yakini huwa umekwishafanyika dhidi yao. Hivyo, watu hao kwa sababu ya kutofanikiwa kwao hawawezi kuitambua alama hii ya mwaminio mkamilifu, bali wanazidi katika shaka, na kwa sababu ya kukosa kwao mafanikio hawawezi kutambua sifa za kukubaliwa maombi za mwaminio kamili. Na ingawa daraja na

cheo cha mwaminio mkamilifu mbele ya Mwenyezi Mungu huwa ni kikubwa, na kwa ajili yake na kutokana na maombi yake ya unyenyekevu kazi kubwa zenye matatizo hurekebishwa, bali baadhi ya kudura zinazoshabihiana na kudura zisizobadilika, hubadilishwa pia. Lakini zile kudura zilizokwisha amuliwa zisibadilishwe, hazibadilishwi kwa maombi ya mwaminio mkamilifu, hata kama mwaminio huyo mkamilifu awe na daraja ya Nabii au Mtume. Ilmuradi, kwa kulinganishwa na wengine, mwaminio mkamilifu katika alama hizi nne hupambanuka wazi wazi, ingawa hawezi kupata uwezo kamili daima dawamu na kufanikiwa. Basi, baada ya jambo hili kuthibitika kuwa kwa kulinganishwa na wengine, mwaminio kamili anayo sehemu kubwa ya kupata bishara nyingi, na kukubaliwa dua zake kwa wingi, na kufunuliwa sana mambo ya ghaibu na kujulishwa sana mno elimu za ndani za Kurani, basi hakuna njia bora ya kujaribu mwaminio kamili na mtu mwingine ila ni hii tu ya kuwa wakaguliwe na wachunguzwe kwa njia hii; yaani kama kuna mashaka kwa watu kuwa kati ya hawa wawili nani ni mwaminio mkamilifu mbele ya Mwenyezi Mungu na nani hana ya daraja hii, basi, wajaribiwe kuhusiana na alama hizi nne. Yaani kwa kuweka alama hizi nne kuwa kipimo na kigezo, iangaliwe wakati wa mashindano kuwa mtu yupi

analingana barabara na kipimo hiki na mizani hii na yupi anapungukiwa na ana kasoro.

Sasa viumbe wa Mwenyezi Mungu wawe mashahidi kuwa mimi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hasa na kwa ajili ya kuushindisha ukweli ninakubali kwa moyo wote mashindano haya. Na kwa mashindano, watu ambao wakitaka kuja kupambana nami, nambari ya kwanza miongoni mwao ni ya Sheikh Nadhir Husain wa Delhi aliyewahi kufundisha Kurani na Hadithi kwa zaidi ya miaka hamsini, kisha akaonyesha mfano huu wa elimu na matendo yake kuwa bila kufanya utafiti na uchunguzi wowote akaandika fatuwa ya kunikufurisha. Na akiwachochea vibaya maelfu ya watu wenye tabia ya kishenzi akasababisha wanitolee matusi machafu. Na akamwachia huru Batalawii mithili ya mbuai mwenye wazimu kwa kufoka akikufurisha na kulaani, na mwenyewe akajigamba kuwa mwaminio kamili, sheikh wa kote pote, na sheikh wa Arabuni na wa Uajemi. Kwa hiyo, huyu ndiye mtu wa kwanza anayeitwa kwenye mashindano. Naam, yeye anayo hiari ya kumleta bwana Batalawii pamoja naye ambaye sasa anadai kupata njozi pia, bali nampa hiari ya kuwajumuisha pamoja naye katika mashindano haya Maulawii Abdul Jabbar mwanaye mtu mwema marehemu Maulawii Abdullah na Maulawii Abdur

Rahman wa Lakhu aliyetangaza ufunuo wake kunihusu kuwa mimi ni mpotevu kwa kudumu na amekwisha toa fatuwa ya kunikufurisha, na pia Maulawii Muhammad Bashir wa Bhopal ambaye ni miongoni mwa wafuasi wake. Lakini Bwana Sheikh, kama ilivyo kawaida yake, akihepa, basi hao mabwana waliotajwa hapo juu wajitokeze mbele yangu. Na kama hao wote wakisita, basi Maulawii Rashid Ahmad Gangohi apige moyo konde kujitokeza, maana yeye ndiye mwanakundi wa kwanza wa kundi la Masuni. Pamoja naye yeyote anaweza kushiriki ambaye ni miongoni mwa masufii, vizazi wa masufii na warithi wa masufii maarufu, na sawa na hawa Masheikh ananichukulia mimi kuwa kafiri, mzushi, mwongo na mjanja. Na kama hao wote wahepe kushindana na kwa kutoa udhuru mbovu usioingia akilini wasite kabisa kuukubali mwito wangu huu, basi hoja ya Mungu imekwishatimia juu yao. Mimi nimetumwa na nimepewa bishara ya ushindi. Hivyo, ninawaita mabwana waliotajwa juu kwenye mashindano. Je yuko yeyote atakayekuja mbele yangu? Na njia bora ya mashindano ni hii kuwa katika Lahore ambayo ndiyo makao makuu ya Mkoa wa Panjab, kamati fulani iundwe kwa ajili ya mtihani huu. Kama kundi la wapinzani likikubali shauri hili, hapo wajumbe wa kamati wachaguliwe kwa

maridhiano ya makundi mawili, na wakati wa hitilafu, rai ya wengi itazingatiwa. Na itakuwa vema kwamba kwa kujaribu kikamilifu alama zote nne, makundi yote mawili yaendelee kuitumia kamati maandishi yao kwa kuweka tarehe mpaka mwaka mmoja. Na kutoka kamati itatumwa risiti za kupokea maandishi pamoja na kuweka tarehe na maelezo ya madhumuni.

Alama ya kwanza, yaani njia ya kujaribu bishara itakuwa hii kwamba makundi mawili watakaodhihirishiwa bishara yoyote kutoka kwa Mungu kwa njia ya ufunuo na kashfi na kadhalika, ifikishwe kwa kamati baada ya kuweka tarehe na ushahidi wa Waislamu wanne kabla ya kutokea kwake. Na kamati iiandike pamoja na tarehe katika rejista yake na kisha wajumbe wote wa kamati au angalau wanakamati watano waweke saini zao, kisha risiti yake moja itumwe kwa mletaji wake sawa na maelezo ya juu. Na ukweli au uongo wa bishara hiyo usubiriwe, na wakati wa kudhihiri kwa matokeo yoyote, liandikwe kumbukumbu lake pamoja na ithibati yake ndani ya rejista na shuhuda za wajumbe ziwekwe juu yake kama kawaida.

Na kuhusiana na alama ya pili pia, ihusuyo matukio na misiba ya duniani, mpango huo utafuatwa. Na izingatiwe kuwa hayo yote yatahifadhiwa na kamati kama siri yakiwa ni amana. Na kamati itakiri kwa kula

kiapo kuwa kabla ya kufichuliwa mambo hayo kwa kulinganisha pande zote mbili katika mkutano wa hadhara, jambo lolote lile hataambiwa mtu yeyote mwingine, isipokuwa kama kufichuka kwa siri iwe nje ya uwezo wa kamati.

Na alama ya tatu yaani njia ya majaribio ya kukubaliwa kwa maombi itakuwa ni kwamba kamati hiyo hiyo itatangazia kote kote kwa kuwaleta waliopatwa na misiba ya aina aina ambamo mtu wa kila dini anaweza kushiriki, na mtu wa kila dini awe Mwislamu au Mkristo au Baniani au Myahudi, ilmuradi awe mwenye kufuata dini yoyote au rai yoyote, kama ameshikwa na msiba mkubwa sana na ajilete katika kundi la wenye msiba, basi atakubaliwa bila ubaguzi wowote. Kwani, Mwenyezi Mungu Hakuweka ubaguzi wowote na tofauti katika kuwanufaisha watu wa dini mbalimabali kimwili na kidunia. Na nidhamu hii itaendelea ya kuwaleta wapatwao na misiba hadi muda wa mwezi mmoja au vile kamati inavyoonelea kwamba vyeti vyao vyenye majina yao na ya baba zao, makazi yao na kadha wa kadha, viendelee kukusanywa katika sanduku moja. Baadaye majina yao yakiorodeshwa katika orodha mbili kwa usawa na kwa kuweka ubini, kabila, makazi, dini, kazi na maelezo ya balaa iliyotokea, zitawekwa mbele ya makundi yote mawili pamoja na wenye

misiba. Na makundi mawili yakichunguza wenye misiba yatazigawa orodha hizo mbili kwa kupigiwa kura. Na endapo kuna mwenye msiba anayeishi katika nchi ya mbali na kutokana na umbali wa safari na kukosa uwezo asiweze kuhudhuria, basi tawi moja la kamati lifunguliwe huko anakoishi huyo mwenye msiba na tawi lile litapeleka maelezo ya msiba wake kwenye kamati kuu. Na baada ya kupigiwa kura kila kundi litakalopewa orodha, katika orodha hiyo wenye misiba waliosajiliwa humo watahesabiwa kuwa sehemu ya kundi lile ambalo Mwenyezi Mungu Amelipa orodha hii kwa kupigwa kura. Na kamati itawajibika kwamba itangaze wiki chache mapema kwa kuleta wenye misiba na kwa lengo la kuhudhiria kwao kwa tarehe iliyopangwa. Na gharama yote ya matangazo hayo itakuwa juu yangu[23]. Na kamati pia itaweka ofisini mwake nakala moja moja ya orodha hizo mbili za wenye misiba, na siku hiyo itahesabika ndiyo siku ya kwanza ya mwaka utakaopangwa. Kila kundi litaendelea kuwaombea wale wenye misiba wa sehemu yake, na sawa na mpango ulioelezwa mambo yote yataendelea kuandikwa katika rejista. Na kama

---

**23** Maelezo ya Pembeni: Maandishi haya yaliposomwa mkutanoni ndugu Maulawii Ghulam Qadir Fasih, Mmiliki na Msimamizi wa Gazeti la Panjab Gazette, Sialkot, akaeleza kimaandishi kwamba gharama yote kwa kuchapisha na kutangaza matangazo haya itakuwa juu yake. Mungu Ampe malipo bora. Mwandishi

mmojawapo akifariki[24] katika muda wa mwaka mmoja au hata kabla ya wakati wa kuweza kukisiwa wingi wa maombi yake kukubaliwa na ushindi wazi, hata hivyo huyo atahesabika kuwa ameshindwa, kwani Mungu Mtukufu kwa shabaha yake maalum alifanya kazi yake isikamilike ili Adhihirishe kuwa yeye alikuwa juu ya batili. Na kundi kubwa la waliopata misiba limewekwa kuwa sharti kwa sababu majaribio ya kupokelewa kwa maombi yanaweza kufanyika kwa njia ya wingi tu. Waila vile tulivyoeleza inawezekana kwamba kama wanaoombewa wakiwa wachache tu, kwa mfano wakiwa watu wawili au watatu tu, kisha wawe na takdiri iliyokwisha amuliwa katika kushindwa kwao, yaani tangu azali iliamuliwa kuwa hawa hawataepukana kabisa na majanga yao, na hali hii ilikuwa ikiwakuta hata Mawalii wakubwa na Manabii kuwa baadhi ya watu walikosa athari ya maombi yao, sababu yake ilikuwa ni hii tu kwamba wao walikuwa na takdiri iliyoamuliwa ya kushindwa, hivyo kumchukua mwenye shida mmoja au wawili kuwa kipimo cha majaribio ni njia ya kutilia mashaka. Maana inawezekana hao wawe na takdiri iliyoamuliwa kwamba watashindwa. Basi wakimwelekea mtawa fulani kwa ajili ya kuombewa, na wasipofanikiwa kwa sababu ya takdiri yao

24 Na kuacha mambo yote ya mashindano bila kutimiza. Mwenezi.

iliyoamuliwa tayari, hapo kupokelewa kwa maombi ya mtawa yule kutafichika kwao, bali pengine wakielekeza fikara yao kwenye dhana mbaya watakosa itikadi juu ya huyo mtawa na kuharibu akhera yao pia pamoja na dunia yao. Kwa majaribio ya aina hii baadhi ya watu walijikwaa katika zama za mitume pia, na wakafikia hata hali ya kuritadi. Na jambo hili ni maarifa ya kina kwamba kukubaliwa kwa waliomkurubia Mungu kunatambuliwa kwa wingi wa maombi yao kukubaliwa. Yaani maombi yao mengi hukubaliwa, siyo kwamba maombi yote yanakubaliwa. Hivyo, mpaka idadi ya wanaokuja kuombewa iwe nyingi, kukubaliwa kwa dua hakuwezi kujulikana. Na uhakika wote na adhama ya wingi hujulikana vizuri wakati mwaminio kamili anayekubaliwa sana dua anapolinganishwa na mwingine, waila yumkini kuwa katika mtazamo wa mpinzani mwovu wingi huo pia uonekane kuwa uchache. Hivyo, kwa kweli kupokelewa maombi kwa wingi kwa mtu ni jambo la kupimika kwa kulinganishawa na mtu mwingine, ambalo utambuzi wake sahihi na wa yakini unaofunga domo la mkataaji hudhihirika kwa mashindano tu. Kwa mfano, kama watu elfu moja moja wenye matatizo wakipewa watu wawili wanaodai kuwa waaminio kamili na wenye kukubaliwa dua zao, na athari ya kukubaliwa kwa

maombi ya mmoja wao iwe hii kwamba miongoni mwa elfu moja wabakie hamsini au ishirini na watano tu ambao wasifaulu na wengineo wote wafaulu, na kutoka katika kundi la pili labda hamsini au ishirini na watano ndio wasalimike kushindwa na waliobakia wote washindwe, basi bila shaka tofauti itakuwa wazi kabisa baina ya aliyekubaliwa na aliyekataliwa. Dhehebu la wasiomwamini Mungu la zama hizi linaonekana kukumbwa na dhana na wasiwasi huu kuwa kwa vile tangu azali imekwisha kadiriwa mambo fulani kufanyika na mambo fulani kutofanyika, hivyo kukubaliwa kwa dua si kitu chochote, lakini mashaka haya ni bure tu kabisa. Na jambo la kweli ni hili tu kuwa kama vile Mwenye hekima kamili Ameweka athari ndani ya dawa ingawa kanuni za asili zimekwisha pangwa, vivyo hivyo ndani ya maombi pia kuna athari zinazothibitika baada ya kufanyiwa majaribio sahihi. Na kama vile Huyu Mwenye baraka Aliye sababu ya sababu zote, Alivyofanya ya kupokea dua tangu zamani kuwa suna yake ndivyo hivyo Huyo Mtukufu Alivyoweka suna yake hii pia kwamba waliokumbwa na matatizo ambao wameamuliwa kuachiliwa tangu awali huachiliwa kwa baraka za maneno matakatifu ya watu hawa hawa au maombi na maelekezo ya moyo wao au uwepo wao ardhini ambao wamejaaliwa na heshima ya kumkurubia

Mungu na kukubaliwa naye. Ingawaje duniani kuna watu wengi pia wanaoabudu masanamu ambao wakati wa matatizo yao hawamwelekei mwaminio mkamilifu, na pia wako wengine wasioamimi kupokelewa kwa maombi, na mategemeo yao ni tadbiri pekee na vifaa, na kwa kuangalia maisha yao mtu mwenye mawazo mafupi anaweza kudanganyika ya kwamba matatizo yao pia yanatatulika. Basi, yawezaja kuthibitika kwa uwazi kwamba maombi ya wateule tu yanakubaliwa kwa wingi. Jibu la wasiwasi huu lililoelezwa ndani ya Kurani Tukufu ni hili kwamba ingawa mtu fulani kwa ajili ya kupata miradi yake alielekee sanamu au miungu mingine au tadbiri zake, lakini kwa kweli, kanuni takatifu ya Allah ni hii hii kuwa mambo hayo yote yanatokana na athari za wateule, na kwa pumzi zao takatifu na kwa baraka zao dunia hii inaendelea kukaliwa. Kwa baraka zao mvua zinanyesha, na kwa baraka zao amani inabaki duniani, na maradhi ya kuambukiza hutoweka na ufisadi unaondolewa. Na kutokana na baraka zao watu wa dunia hufanikiwa katika tadbiri zao. Na Kwa baraka zao mwezi unatoka na jua huangaza. Hao ni nuru ya ulimwengu na dunia hung'ara maadamu waja wa aina yao wapo duniani, na dunia itafikia mwisho wake pamoja na kumalizika waja wa aina hii, kwani hao ndio jua na mwezi wa kweli wa ulimwengu.

Kwa maneno hayo ni wazi kwamba miradi ya binadamu bali tegemeo la maisha ni watu hao, na sio wanadamu tu bali hao ndio msingi wa uthabiti wa kila kiumbe na uzima wao. Kama hao hawapo, basi angalieni masanamu yatafaa nini na kuna faida gani ya tadbiri? Hii ni siri ya ndani sana ambayo kuifahamu hiyo akili ya hapa duniani pekee haiwezi kutosha, bali inahitajika ile nuru wanayoipata wenye maarifa ya kiroho. Kwa kweli shaka zote hizi, huondolewa kwa njia ya mashindano. Maana, wakati wa mashindano Mwenyezi Mungu Huwa na utashi maalum kwamba idhihirike heshima ya yule mwenye kukubaliwa kwa kweli na mwenye baraka za kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kama anayeabudu masanamu ashindane na mwenye imani katika Umoja wa Mungu, nao watahiniane katika kupokelewa maombi, atadhalilika sana anayeabudu masanamu. Ndiyo maana mimi nilisema hapo kabla pia kuwa hakuna njia rahisi ya kumpima mwaminio mkamilifu kuliko kufanya mashindano. Kama kuhusu jambo fulani dua ya mwaminio mkamilifu isikubaliwe na awe amejulishwa kuhusu kutokubaliwa huku kwa njia ya ufunuo wa Mungu, hapo jambo hilo litashindikana hata kama tadbiri zote za Amerika na Ulaya ziishie au masanamu yote ya duniani yasujudiwe, au dunia nzima iombe mafanikio katika jambo hilo. Na ingawa

baraka ya mwaminio mkamilifu inafanya kazi duniani, na kwa baraka yake tu nidhamu ya dunia inaendelea, na ndani kwa ndani huwa ndiyo njia ya kupata miradi ya kila mtu hata kama mtu akimfahamu au asimfahamu. Lakini wale watu wanaoelekea kwake kwa upendo na ikhlasi, hao siyo tu kuwa wanafikia miradi yao ya kidunia kwa baraka yake bali hurekebisha hata dini yao pia na huimarisha imani zao na kumtambua Mola wao. Na kama wakiendelea kukaa pamoja na mwaminio mkamilifu kwa uaminifu na wasikimbie katikati, basi wanapata kushuhudia ishara za mbinguni kwa wingi sana.

Na hii sharti ya kuwepo kwa wenye shida za aina mbalimbali, niliyoandika ndani ya madhumuni hii, nimeiandika ili rehema ya Mwenyezi Mungu idhihirike kwa kawaida katika sura ya namna mbalimbali na mtu wa kila tabia na hali aweze kuielewa. Na wanaweza kuelewa wenye misiba ya aina mbalimbali kwa mifano ifuatayo: Kwa mfano, mtu fulani anayo maradhi ya aina mbalimbali, na fulani amenasa katika adhabu fulani bila haki au anaelekea kunasa, na fulani ambaye mwanaye mpendwa amepotea asijulikana habari zake, na fulani mwenyewe hana kizazi, na fulani amepata dhila ya kustahili kuhurumiwa baada ya kupata heshima na cheo, na mwingine amepata kudhulumiwa na

dhalimu fulani, na mwingine kwa kulemewa na deni kubwa sana zaidi ya uwezo wake yupo katika hali mbaya, na mwana wa mwingine awe ameritadi kutoka dini ya Uislamu, na pengine fulani amepatwa na huzuni na taabu tusiyoweza kuielezea wakati huu.

Alama ya nne, yaani kufunguliwa maarifa ya ndani ya Kurani Tukufu, kuhusu jambo hili mpango mzuri ni huu ya kuwa kila mshindani kwa kuandika elimu ya ndani, hakika, na maelezo ya kina ya Aya chache za Kurani ayasome mbele ya kamati katika mkutano wa hadhara, kisha maelezo yaliyoandikwa yakithibitika kuwa yalikuwa yameandikwa ndani ya kitabu fulani cha zamani cha maelezo ya Kurani, mtu huyo kwa kuhesabiwa kuwa ni mwenye kunakili tu akemewe. Lakini kama mambo aliyoeleza ya hakika na maarifa ya ndani yenyewe ni sahihi bila makosa yoyote na pia yawe mapya ambayo wafasirina waliotangulia hawakuyawaza, na hata hivyo maana hizo si za kujikalifisha kwa kila jiha, na zidhihirishe mwujiza wa Kurani Tukufu na adhama ya hali ya juu na shani yake, na ndani mwake mna utukufu, heba na nuru ya ukweli, basi yafaa kufahamu kuwa hayo ndiyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambayo kwa kudhihirisha heshima ya mpendwa wake na kukubaliwa kwake na umahiri wake Amempa elimu kutoka kwa elimu Yake Mwenyewe. Hivi ndivyo vigezo vinne vya kutahini

nilivyoandika, navyo ni safi na vilivyonyoka. Kila mtu atakayevizingatia atakubali kuwa hakuna njia nyingine ya kiroho iliyo safi na rahisi ya kuamulia baina ya wagomvi wawili. Ninakiri kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu kuwa kama mimi nikishindwa katika mashindano haya, mimi mwenyewe nitachapisha ikirari ya upotofu wangu. Hapo Sheikh Nadhir Husain na sheikh Batalawii hawatakuwa na haja ya kunikufurisha. Na katika hali hii mimi ndiye nitastahili kila dhila, shutuma na fedheha na nitakiri katika mkutano huo huo kuwa mimi sikutoka kwa Mwenyezi Mungu na madai yangu yote ni batili. Na wallahi nina yakini na ninaona kuwa Mungu wangu kamwe Hatafanya hivyo na Hataniacha nipotee bure. Sasa kukwepa kwa wanazuoni waliotajwa hapo juu (kama wakiukwepa) mtihani huu bayana na wazi haitakuwa tu kinyume cha uadilifu bali katika rai yangu wao kwa kunyamaza au kutosheka na majibu ya udanganyifu yasiyokuwa sahihi watawafanya watu wenye busara wawadhanie vibaya sana. Hao kama wakitoa majibu ya kuhadaa yaliyojaa hila kwa kumkabili mtu ambaye kwa moyo wa kweli amesimama katika medani kwa kushindana, basi wakumbuke kuwa mtu yeyote anayeutafuta ukweli na kuupenda hatapendezwa na jibu la aina hii; bali waadilifu watalisikitikia.

Inawezekana wazo likazuka moyoni mwa mtu kwamba yule anayedai kuwa Masihi Mau‘udi kwa nini haonyeshi mwenyewe kwa upande wake ishara za kuwatuliza watu? Jibu lake ni hili kuwa watu wote hawa wanawafuata maulamaa, na maulamaa hao wamekwisha eneza baina ya watu kwa njia ya vipeperushi vyao kuwa mtu huyu ni kafiri, dajali, hata kama akionyeshe ishara nyingi namna gani, hastahili kukubaliwa. Ndiyo maana, Sheikh Batalawii katika kipeperushi chake kirefu alichochapisha baada ya majadiliano ya Ludhiana aliandika maneno hayo waziwazi, na akaeleza kuhusiana nami kwa chuki na uhasama kuwa mtu huyu anayetoa mwito wa kuonyesha ishara za Kimbingu, watu hawatakiwi kuujali mwito wake, kwani hata Ibni Sayyad pia alionyesha ishara, na dajali aliyeahidiwa pia atazionyesha; basi ishara hazitegemewi. Mbali na haya, mimi ninasikia pia na kusoma ndani ya matangazo ya wapinzani wangu, kuwa ishara zilizo za upande wangu pekee wanaziangalia kwa mtazamo wa dharau, na kwa kukorofisha wanasema kuwa kama mtu huyu akielezea ndoto yake ya kweli au adhihirishapo bishara ya ufunuo, ana sifa gani ya kupambanua katika mambo haya? Makafiri pia huota ndoto za kweli, bali pengine hata dua zao pia hukubaliwa, nao wakati mwingine wanapata kujua

jambo fulani kabla ya kutokea kwake, wengine kwa kula kiapo husema kuwa mambo haya hata sisi tunayo pia. Na hawajui kuwa kwa dirhamu moja fukara hawezi kuitwa tajiri, na kwa mwanga wake kidogo kimemeta hawezi kuitwa jua. Lakini bila mashindano watu hao hawawezi kufahamu. Wakati wa mashindano wakishindwa wanayo hiari ya kuwashirikisha pamoja nao makafiri kumi au ishirini hivi. Ilmuradi, maadamu masheikh hawakubali kabisa ishara za upande mmoja pekee na wananitambua kuwa kafiri tu, wanachukulia ishara zangu kuwa ni kiinimacho au kuzitazama kwa mtazamo wa dharau, basi, alama za upande mmoja tu zitaleta athari gani? Na watu ambao mioyo na masikio yao yametiliwa maneno hayo, vipi watatulia na ishara hizi? Lakini mashindano ya kuonyesha ishara za kiimani ni njia safi yenye mwanga ambamo hauwezi kuletwa udhuru wa maulamaa hao. Na kiasi ukweli unachodhihirika wazi wazi wakati wa mashindano, kiasi hicho haki haiwezi kudhihirika kwa njia yoyote nyingine. Naam, kama watu hao hawana uwezo wa kushindana huku, basi ni wajibu wao wachapishe tangazo kwa kuafikiana kwa kuweka mihuri yao kuwa sisi hatuwezi kushindana, na alama za waaminio wakamilifu hazimo ndani mwetu. Na waandike pia kuwa tunakiri kwamba sisi bila udhuru wowote tutazikubali baada

ya kuziona ishara za huyu mtu, yaani mimi, na tutawasihi pia watu wazikubali. Isitoshe, tutayakubali madai yake pia na tutajiepusha na njama za kishetani za kumkufurisha, na tutamtambua kuwa yu mwaminio kamili. Hapo naahidi kuwa kwa fadhili za Allah Mwenye shani nitatoa uthibitisho wa ishara za upande wangu pekee. Na ninatumaini kwamba Mungu Mwenye nguvu na uwezo Atawaonyesha ishara zake, na Atakuwa Mwenye kumhami na kumsaidia mtumishi wake, na Atatimiza ahadi zake kwa kweli na haki. Lakini, kama watu hao wasichapishe maandishi kama hayo, basi hapo kwa vyovyote vile kufanya mashindano ndiyo afadhali, ili fikara yao na kiburi chao kipate kuamuliwa kuwa sisi ni waumini kamili, ni masheikh wa kote kote na viongozi wa zama, tena ni wenye kupokea funuo na kupewa heshima ya maongezi na Mungu, lakini mtu huyu ni kafiri, dajali na ni mbaya kuliko mbwa. Na katika mashindano haya kuna faida nyingine hii pia kwamba uamuzi wa upande wetu mmoja unaohitaji muda mrefu, uamuzi huo kwa njia ya mashindano utafanyika katika siku chache tu. Kwa hiyo, mashindano haya ni njia rahisi sana na ni ya karibu zaidi kwa kuuamulia ugomvi huu kwamba nani ni mumini kikweli na nani anayo sera ya makafiri. Kwa njia hii ugomvi utakwisha haraka, kana kwamba

masafa ya mamia ya maili yatafupika yakawa kama hatua moja. Na ghera ya Mwenyezi Mungu itadhihirisha haraka sana kuwa uhakika hasa ni upi. Na faida nyingine ya mashindano haya ni kwamba kwa njia hii pande zote mbili hazibaki na sababu ya kutoleana makosa, wala hakuna mwanya wa kutoa udhuru usiokuwa wa haki. Lakini katika ishara za upande mmoja pekee, upinzani wa mtu mwovu huwafanya watu wa kawaida kudanganyika. Wajuao wanajua pia kuwa mpaka leo ishara nyingi za upande mmoja pekee zimeisha dhihirika kutoka kwangu ambazo waliozishuhudia wako hai. Lakini je, juu ya kuzithibitisha, masheikh watazikubali? La, hasha! Na ikumbukwe pia kwamba maneno haya yote na njia hii iliyochaguliwa, ndiyo kwa kutaka uamuzi wa haraka kwa ajili ya wakataaji, na kwa ajili ya kuwanyamazisha na kuwafumba midomo yao na kwa nia ya kuwatimizia haja na kuonyesha dhihirisho kamili la ukweli na kufikisha ujumbe huu niliopewa na Mungu. La sivyo, kudhihiri kwa ishara hakuhusikani na mashindano ya hao, bali ishara zinaendelea kudhihiri tangu mwanzo. Na kila anayekaa nami sharti akae kwa ukweli na uthabiti, anaweza kuona ishara kiasi fulani. Na hata baadaye pia Mwenyezi Mungu Hataiacha Jumuiya hii bila kuonyesha ishara wala Hataacha kusaidia. Bali kama zilivyo ahadi zake

tukufu, Yeye Ataendelea kuonyesha ishara mpya mpya kwa nyakati zake mpaka awe ametimiza hoja yake na kupambanua baina ya habithi na taibu. Yeye Mwenyewe katika maongezi yake Akasema kunihusu mimi kuwa Mwonyaji mmoja akaja duniani, lakini dunia haikumkubali; wa lakini Mungu Atamkubali na Atadhihirisha ukweli wake kwa mashambulizi makali sana. Nami siwezi kutumai kuwa mashambulizi yale hayatatokea, ingawa sina madaraka katika kudhihiri kwake. Nawahakikishieni kuwa mimi ni mkweli, enyi wapendwa! Eleweni kuwa Mungu wa mbingu na ardhi Asipokuwa pamoja na mtu, yeye hawezi kuonyesha ushujaa wa aina hii kuwa asimame imara kuikabili dunia na adai madai yaliyo nje ya uwezo wake. Yule mtu anayesimama imara na kwa nguvu kuikabili dunia, je yeye anaweza kusimama mwenyewe? La, hasha. Bali yeye husimama chini ya himaya ya Mweza na kwa kutegemea mkono wa ghaibu, Ambaye ardhi na mbingu zote na kila roho na mwili upo chini ya madaraka yake. Hivyo, fumbueni macho na fahamuni kuwa yule Mungu ndiye Aliyenipa mimi mnyenyekevu nguvu na uimara huu, Ambaye ninayo heshima ya kuongea naye. Kutoka kwake na kwa amri yake iliyo wazi nimejasiri kusimama kwa ushujaa mkubwa na uimara wa moyo kuwakabili hao watu wanaodai kuwa tu viongozi na

masheikh wa Arabuni na Uajemi na tuko karibu na Mungu, na humo mna kundi la wanaojiita wenye kupokea funuo na wanadai kuongea na Mungu, na kwa dhana zao wamekwisha niamulia kwa ufunuo wao kuwa mimi ni kafiri na mtu wa motoni. Basi, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu mimi nimekuja katika medani kuwakabili hao wote ili Mwenyezi Mungu Apambanue baina ya mkweli na mwongo, na ili Mkono wake umdhalilishe mwongo, na ili Amnusuru na Amsaidie yule aliyemfadhili. Hivyo, enyi ndugu, angalieni, wito huu ninaowatolea Sheikh Nadhir Husain na wenzake, kwa kweli ni njia ya wazi ya kuhukumu kati yangu na hao. Hivyo, mimi nimesimama katika njia hii. Sasa kama machoni mwa maulamaa hao, mimi ni kafiri wa ania hii, na dajali, na mzushi na mwenye kupotoshwa na shetani, basi kwa nini wanasita kunikabili? Je hawakusoma ndani ya Kurani Tukufu kuwa wakati wa mapambano msaada wa Mungu huwa pamoja na waumini tu. Mungu Mwenye shani Anasema ndani ya Kurani Tukufu وَلَا تَهِنُوْا وَلَا تَحْزَنُوْا وَ اَنْتُمُ الْاَعْلَوْنَ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ[25] yaani, Enyi waumimi, msilegee katika mashindano wala msiwe na wasiwasi, hatimaye ushindi ni wenu. Na Anasema وَلَنْ يَّجْعَلَ اللّٰهُ لِلْكٰفِرِيْنَ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ سَبِيْلًا[26]. Yaani,

**25** Aal Imraan, 3: 140. Mwenezi.
**26** An-Nisaa, 4:142. Mwenezi.

Mwenyezi Mungu Hatawajaalia makafiri njia ya kuwashinda waaminio. Hebu angalieni, Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu Amewapatia waaminio bishara ya ushindi wakati wa kukabiliana. Na ni dhahiri kuwa Mwenyezi Mungu Humhami na kumsaidia mwaminio tu, kamwe Hawezi kumsaidia na kumhami mzushi. Hivyo, yule ambaye Mwenyezi Mungu Mwenyewe ndiye adui wake na Anajua kuwa yu mzushi, vipi mtu mbovu kama huyu anaweza kujaaliwa heshima ya kuwa na alama maalum za imani akikabiliana na mwaminio! Inawezekanaje kuwa marafiki wapendwa wa Allah, warithi wa kweli wa kupata funuo za Allah, tena ndio waaminio wakamilifu na ni masheikh wa kote pote, wanyimwe wakati wa mashindano ishara za kiimani na wapate kuaibika kwa dhila kubwa, na Mwenyezi Mungu makusudi Avunje utukufu na sifa zao njema, lakini yule aliyefukuzwa katika kizingiti cha Mungu, na sawa na kauli ya sheikh Batalawii ni kama mbwa na kafiri na dajali, na kwa kauli ya Sheikh Nadhir Husain yu mtu asiye na imani kabisa, na ni mpotevu na mbaya kuliko viumbe wote, ndani yake alama za imani zipatikane, na wakati wa mapambano Mwenyezi Mungu Ampe huyu huyu ushindi na ufaulu. Haiwezekani kufanyika hivi. Enyi wasomaji, kwa imani yenu hebu elezeni, je msaada wa kimbingu

na wa kiroho huwa kwa ajili ya waaminio au kwa ajili ya makafiri? Katika mazungumzo haya yote nimeshathibitisha kwamba kwa kupambanua kwa uwazi haki na batili, mashindano yanahitajikia sana, تاسیہ روئے شود ہر کہ دروغش باشد[27] Mimi nimevumilia sana matusi machafu ya sheikh wa kote pote na wanafunzi wake, na nimesumbuliwa na niliendelea kujizuia. Sasa kwa sababu ya kutumwa nawatolea sheikh wa kote kote na kundi lake mwito huu wa Mungu, nami nina yakini kuwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe Atautolea uamuzi ugomvi huu. Yeye ndiye Anayeyachambua mawazo ya mioyoni, na kukagua mambo yaliyomo vifuani, na Hapendi kwa mtu uhalifu wenye kuumiza moyo na kusema jambo baya hadharani. Yeye Hajali. Mcha Mungu ni yule anayemwogopa. Mimi navunjiliwaje heshima kama mtu akiniita mbwa au kafiri-kafiri, na dajali? Kwa kweli mtu ana heshima gani? Heshima hupatikana kwa kumwangukia mtu miali ya nuru Yake. Kama Yeye Hakuniridhia, na mimi ni mbaya machoni mwake, hapo siyo tu kwamba mimi ni kama mbwa, bali ni mbaya mara elfu kuliko majibwa.

[27] Ili kila aongopaye apate kudhalilika. Mwenezi.

گر خدا از بندۂ خوشنود نیست　　هیچ حیوانے چو او مردود نیست[28]

گر سگِ نفسِ دنی را پروریم　　از سگانِ کوچہ ہا ہم کم تریم

اے خدا اے طالبان را رہنما　　ایکہ مہر تو حیاتِ روح ما

بر رضائے خویش کن انجام ما　　تا براید در دو عالم کام ما

خلق و عالم جملہ در شور و شراند　　طالبانت در مقام دیگر اند

آن یکے را نورے بخشی بدل　　واں دِگر را می گزاری پابگل

چشم و گوش و دل زِ تو گیرد ضیاء　　ذات تو سرچشمۂ فیض و ہُدا

Ilmuradi, Mungu Mweza na Mtukufu ndiye kimbilio langu, na ni ninamkabidhi Yeye kazi yangu yote. Sitaki kutusi nitusiwapo, wala sitaki kusema lolote;

---

[28]Mungu Asipomridhia mtu, hata hayawani si mbaya zaidi kuliko yeye.

Kama tunajishughulikia kulisha mbwa wa nafsi yetu dhalili, basi tu wabaya zaidi kuliko mbwa za mitaani.

Ee Mungu, Ee Mwongozi wa watafutao njia, Ewe Ambaye Upendo wako ndio uhai wa roho yetu.

Utujaalie mwisho wetu uwe kwenye radhi yako, ili utashi wetu uwe umetimia.

Dunia na watu wake wote wanashughulikia makelele na fujo, lakini wakutafutao wako katika hali nyingine kabisa.

Mmoja wao katika hao Unamjaalia moyo wake mwanga, na mwingine Unamwacha katika matope.

Macho, masikio na nyoyo hujipatia nuru kutoka kwako tu, Dhati yako ndiyo chemchem ya baraka na mwongozo. Mwenezi.

Yupo tu Mmoja Atakayesema. Ni masikitiko kuwa watu hao wamelipeleka mbali sana jambo lililokuwa dogo na hawakumtambua Mwenyezi Mungu kuwa Mwenye uwezo wa kufanya Atakavyo na kumtuma Amtakaye. Je mtu anaweza kupigana naye au mwanadamu anayo haki ya kumpinga Yeye kwamba kwa nini Umefanya hivi na kwa nini Hukufanya vile? Je Yeye Hawezi kumjaalia mwingine nguvu na tabia ya mtu fulani, na rangi na hali ya mmoja kumpatia mwingine na kumpa mtu fulani jina la mwingine? Kama mtu ana imani juu ya uwezo wenye wasaa wa Mwenyezi Mungu, bila kusita yeye atatoa jawabu lake kwamba 'Ndiyo, bila shaka Mungu Mwenye shani Anao uwezo juu ya kila kitu, na Anaweza kutimiza maneno yake na bishara zake kwa namna na njia yoyote ile Anayoipenda.' Wasomaji, hebu, fikirini nyinyi wenyewe kuwa je kuna mahali popote palipoandikwa kumhusu Isa anayekuja kuwa atakuwa ni yule yule Mnazareti mwana wa Israeli mwenye Injili? Bali ndani ya Bukhari iitwayo kitabu sahihi zaidi baada ya Kurani Tukufu, badala ya maneno hayo imeandikwa:

امامكم منكم[29] na imetoa ushahidi wa kifo cha Hadhrat Masihi[as]. Mwenye macho na aone. Enyi waadilifu!

[29] Ni Imam wenu kutoka miongoni mwenu. Mwenezi.

jibuni kwa kutafakari kwamba je imeandikwa popote ndani ya Kurani Tukufu kuwa atadhihiri mvunja misalaba kidhahiri, na mwuaji wa raia wasiokuwa Waislamu waishio katika nchi ya Kiislamu, na mwenye kuleta amri mpya ya kuwaua nguruwe na ni mwenye kutangua baadhi ya maagizo ya Kurani Tukufu, na wakati huo aya [30] اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ na aya[31] حَتّٰى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَنْ يَّدٍ zitatanguka, na wahyi mpya utaufuta wahyi wa Kurani Tukufu. Enyi watu, Enyi mnaojiita dhuria za Waislamu, msiwe maadui wa Kurani na baada ya Khaatamun Nabiyyiin msianzishe silsila mpya ya wahyi wa unabii, na mwoneeni haya Mungu mtakayehudhurishwa mbele yake.

Mwishoni, mimi napenda kuwaarifu wasomaji kuwa mambo yaliyomfanya Bwana Maulawii Nadhir Husain na kundi lake wanitolee fatuwa ya kunikufurisha na kuniita kafiri na dajali na kunitolea matusi ambayo mtu mstaarabu hawezi kupenda kumtolea hata mtu wa dini nyingine, na kudai kana kwamba maneno hayo yameandikwa ndani ya vitabu vyangu *Taudhihe Maraam* na *Izaala Auhaam*. Mungu akijaalia, hivi karibuni mimi nikiandika

**30** Leo nimewakamilishieni dini yenu. Maida, 5:4. Mwenezi.

**31** Mpaka watoe kodi kwa mkono hali wakitii. Tauba, 9:29. Mwenezi.

katika kijitabu kingine sehemu zote zinazopingwa nitawaonyesha waadilifu kuwa je kweli nimetengana na itikadi ya Uislamu au machoni mwao kuna pazia na mioyo yao imepigwa mihuri hata kwamba juu ya kudai kuelimika hawawezi kutambua uhakika. Hao wanawazuia watu mfano wa daraja ambalo likavunjika mara moja na kusababisha maji kufurika kila upande. Kumbukeni kuwa hatimaye watu hao watafumba midomo yao kwa aibu kubwa. Na kwa kuaachana na harara ya kukufurisha watapoa kwa aibu na dhila mithili ya moto uwakao unapomwagiwa maji. Lakini ustadi na busara na akili ya mtu ndiyo ndani ya kufahamu kabla hajafahamishwa, na apate kujua kabla hajaambiwa, kwani kama akielewa baada ya kujibidiisha sana, basi akaelewa nini! Hivi karibuni wengi watafikiwa na zama ambapo baada ya kukufurisha na kutukana watajirudi, na baada ya kufanya dhana mbaya, watakuwa na dhana njema, Lakini thamani ya jambo hilo haiwezi kulingana na thamani ya jambo hili.

اکنوں ہزار عذر بیاری گناہ را    مر شوی کردہ را نبود زیب دختری[32]

Kwa hiyo, enyi watu wangu wapenzi, thaminini

---

[32] Sasa unatoa udhuru elfu za dhambi yako,
Haifai aliyeolewa kujifanya bikira. Mwenezi.

wakati huu. Dhana yenu hii siyo sahihi kabisa kuwa mwanzoni mwa karne hii Mungu wa mbingu na ardhi Hakumtuma Mujadidi yeyote kutoka kwake, bali Akamtuma kafiri na dajali ili aeneze ufisadi duniani. Enyi watu, istahini bishara ya Mtume[saw] na mwogopeni Mwenyezi Mungu, na msiikatae neema.

غافل مشو گر عاقلی دریاب گر صاحب دلی    شاید کہ نتواں یافتن دیگر چنیں ایام را[33]

والسّلامُ علٰی من اتّبع الھدٰی[34]

Tanbihi: Kijitabu hiki cha juu kilisomwa na Maulawii Abdul Karim wa Sialkot katika msikiti mkubwa mjini Qadian mbele ya umati mkubwa, tarehe 27 Desemba 1891, baada ya sala ya Adhuhuri. Baada yake wakaulizwa waliokuwepo rai kuwa watu wepi wafanywe kuwa wanakamati, na namne gani mambo yaanzishwe. Waliohudhuria ambao majina yao yanaorodheshwa hapa chini ambao wakafika kwa kuifikiria rai hiyo hapo juu. Wote hao kwa pamoja waliafiki kwamba kwa sasa kijitabu hiki cha juu kichapishwe na baadaye kwa kujua maoni ya wapinzani, wanakamati wateuliwe kwa ridha ya makundi mawili na kisha kazi ianze. Ndugu

---

**33** Kama u mwenye akili, msighafilike. Kama u mwenye busara unufaike tu, pengine siku hizi hazitaweza kupatikana. Mwenezi.
**34** Na amani iwe kwa waufuatao mwongozo. Mwenezi.

waliohudhuria katika mkutano huu, majina yao ni haya:

Bwana Muhammad Arura, mrasimu katika Korti ya Hakimu, Kapurthala

Bwana Muhammad Abdur Rahman, Karani katika Korti ya Jenerali ya Jeshi, Kapurthala

Bwana Muhammad Habibur Rahman, Tajiri wa Kapurthala

Bwana Zafar Ahmad, Mwandishi wa rufaa, Kapurthala

Bwana Muhammad Khan, Mkuu wa kesi za jinai wa Kapurthala

Bwana Sardar Khan, sajini wa Korti, Kapurthala

Bwana Imdad Ali Khan, Karani katika Ofisi ya Elimu, Kapurthala

Bwana Maulawii Muhammad Husain, Kapurthala

Bwana Hafidh Muhammad Ali, Kapurthala

Bwana Mirza Khuda Bakhsh, mwalimu wa Nawab Malerkotla

Bwana Rustam Ali, Naibu Inspekta wa Polisi wa Reli Lahore

Bwana Haji Seyid Fateh Ali Shah, Naibu Mtoza kodi wa idara ya Mito

Bwana Haji Khwaja Muhammad-ud- Din, Tajiri wa Lahore

Bwana Mian Muhammad Chattu, Tajiri wa Lahore

Bwana Khalifa Rajbuddin, Tajiri wa Lahore

Bwana Shamsuddin, karani wa Ofisi ya Mitihani, Lahore

Bwana Tajdin, Mhasibu wa Ofisi ya Mitihani, Lahore

Bwana Nabii Bakhsh, Lahore

Bwana Hafiz Fazl Ahmad, Lahore

Bwana Maulawii Rahimullah Lahore

Bwana Ghulam Husain, Imam wa Msikiti wa Gumti Lahore

Bwana Abdur Rahman, karani wa Ofisi ya Reli, Lahore

Bwana Maulawii Abdur Rahman wa Msikiti wa Chinian, Lahore

Bwana Karam Ilahi, Lahore

Bwana Seyid Nasir Shah, Naibu Msimamizi wa ujenzi.

Bwana Hafidh Muhammad Akbar, Lahore

Bwana Ghulam Qadir Fasih, Mmiliki na Msimamizi wa Matbaa ya Panjab na Kamishna wa Manispaa ya Sialkot

Bwana Maulawii Abdul Karim, Sialkot

Bwana Mir Hamid Shah Ofisa mwenye madaraka ya kusamehe kodi ya ardhi, Sialkot

Bwana Mir Mahmud Shah, mwandishi wa nakala, Sialkot

Bwana Muhammad Din, mkaguzi mstaafu wa kodi ya ardhi, Sialkot

Bwana Hakim Fazluddin, Tajiri wa Bhera

Bwana Mian Najamuddin, Bhera

Bwana Ahmadullah Muhaldar wa Ofisi ya kibali, Jammu

Bwana Seyid Muhammad Shah, Tajiri wa Jammu

Bwana Umaruddin, mjenzi, Jammu

Bwana Maulawii Nuruddin tabibu mkuu wa Serikali ya Jammu

Bwana Khalifa Nuruddin, mjalidi, Jammu

Bwana Muhammad Akbar, mkuu (mstaafu) wa tarafa, Jammu

Bwana Muhammad Jan, mwajiriwa wa Raja Amar Singh, Wazirabad

Bwana Maulawii Abdul Qadir, Mwalimu Jamalpur

Bwana Sheikh Rahmatullah, Kamishna wa Mansipaa, Gujrat

Bwana Abdur Rahman B.A., Gujrat

Bwana Ghulam Akbar Yatim, karani katika Ofisi ya Mtahini, Lahore

Bwana Dost Muhammad, Sajini wa Polisi, Jammu

Bwana Fazlur Rahman, tajiri, wa Jammu

Bwana Ghulam Muhammad bin Maulawii Din Muhammad, Lahore

Bwana Saiin Sher Shah Majdhub, Jammu

Bwana Iftikhar Ahmad, Ludhiana

Bwana Qadhi Khwaja Ali, kontrakta wa magari, Ludhiana

Bwana Hafidh Nur Ahmad, kiwanda cha hariri, Ludhiana

Shahzada Hadi Abdul Majid, Ludhiana

Bwana Haji Abdur Rahman, wa Ludhiana

Bwana Shihabuddin, Ludhiana

Bwana Haji Nidhamuddin, Ludhiana

Bwana Sheikh Abdul Haq, Ludhiana

Bwana Maulawii Muhkamuddin Mukhtar, Amritsar

Bwana Sheikh Nur Ahmad, mmiliki wa Matbaa Riadhul Hind, Amritsar

Bwana Ghulam Muhammad, Mwandishi, Amritsar

Bwana Mian Jamaludin, Sekhwan

Bwana Mian Imamuddin, Sekhwan

Bwana Mian Khairuddin, Sekhwan

Bwana Maulawaii Muhammad Isa, mwalimu, Naushehra

Bwana Mian Charagh Ali, kijiji cha Ghulam Nabii

Bwana Sheikh Shhabuddin, kijiji cha Ghulam Nabii

Bwana Mian Abdullah, Sohal

Bwana Hafidh Abdur Rahman, Sohian

Bwana Ni'mat Ali Hashimi Abbasi, Batalawii

Bwana Hafidh Hamid Ali, mwajiriwa wa Bwana Mirza

Bwana Hakiim Jan Muhammad, Imam wa Msikiti, wa Qadian

Bwana Babu Ali Muhammad, tajiri, Batala

Bwana Mirza Ismail Beg wa Qadian

Bwana Mian Budde Khan, Mzee wa mtaa, Beri

Bwana Mirza Muhammad Ali, tajiri Patti

Bwana Sheikh Muhammad Umar bin Haji Ghulam Muhammad, Batala

## Mwito Kwa Daktari Jagan Naath, Mtumishi Wa Utawala Wa Jammu Kwenye Ishara Za Kimbingu

Rafiki yangu aliyehalisika na mpendwa kwa ajili ya Mungu, ndugu yangu Bwana Hadhrat Maulawii Hakiim Nuruddin aliyejitupa katika kutafuta radhi ya Mola, mtumishi na tabibu wa serikali ya Jammu alinileteа barua tarehe 7 Januari 1892 ambayo ibara yake kiasi fulani inaandikwa hapa chini, nayo ndiyo hii: "Mimi mnyenyekevu Nuruddin baada ya Assalamu alaikum warahmatullahi wabarakatuh kwa mheshimiwa Hadhrat Masihi wa zama, Rahmani Akuhifadhi, naeleza kwa adabu nyingi kuwa juzi nilikutumia barua, kisha ikatokea taarifa ya kuzuka tufani ya utovu wa adabu hapa Jammu, ambayo naonelea niiandike hapa kwa kirefu. Hudhur, uliandika ndani ya kitabu chako Izaala Auhaam kuhusiana na Daktari Jagan Naath kuwa yeye amekwepa kujitokeza. Sasa Dk. Jagan amewaeleza watu wengi wanaofahamu vizuri jambo hili kuwa jambo hili limeandikwa kwa wino mweusi, lifutilieni mbali kwa kulipigia wino mwekundu. Mimi sikukwepa wala sikutaka ishara yoyote maalum, mimi siombi mfu afufuliwe wala mti uliokauka upate kustawi. Yaani, nataka ishara yoyote iwayo bila sharti

iliyo nje ya uwezo wa mwanadamu.[35]

Sasa iwe wazi kwa wasomaji kuwa katika barua yake ya awali Bwana Daktari aliomba ishara makhsus kama vile kufufua mfu n.k. Nilimwandikia barua kuhusu jambo hili kuwa kuomba ishara makhsus hakujuzu. Mwenyezi Mungu Hudhihirisha ishara zake sawa na utashi na hekima yake. Na kama ishara yenyewe ni

---

[35] Maelezo ya pembeni: Naandika sentensi chache za barua ya Bwana Maulawii, yafaa zisomwe kwa makini ili ijulikane kwamba yeye kwa fadhili ya Rahmani amejaaliwa utulivu kiasi gani na hatua ya ukweli na yakini kamili. Na sentensi zenyewe ni hizi: "Mheshimiwa Bwana Mirza, nipatie nafasi ya kukaa miguuni pako. Nahitaji ridhaa ya Allah na niko tayari kwa chochote kinachomridhisha. Kama ujumbe wako unahitaji umwagiliaji wa damu ya binadamu, basi mimi nisiyefaa kitu (lakini nimpendaye binadamu) nataka kujitolea kwa kazi hii." Maneno yake yameisha, Allah Amjazi. Hadhrat Bwana Maulawii ambaye amejitolea mhanga katika unyenyekevu, adabu, kutolea mali na heshima. Yeye mwenyewe hasemi bali roho yake inasema. Kwa hakika sisi twaweza kuwa watu wakweli wakati ambapo tumrudishie au tuwe tayari kumrudishia Mwenezi Mungu Mwenye kuneemesha kile Alichotupa. Uhai wetu ni amana yake, na Amesema kwamba تُؤَدُّوا الْاَمَانَاتِ اِلٰۤى اَهْلِهَا *

سر کہ نہ در پائے عزیزش رود بارِ گران ست کشیدن بدوش**

---

*Mrudishe amana kwa wanaozistahili.

**Yaani, si miguu bali kichwa kitolewe dhabihu kwa mpendwa, kwani kukibeba mabegani ni kazi nzito sana. Mwenezi.

jambo lililo zaidi ya uwezo wa mwanadamu, basi kuna haja gani ya kuichagua. Kwa kupima ishara yoyote njia hii tu ndiyo inatosha, kuwa nguvu za binadamu zisiweze kuleta mfano wake. Bwana Daktari hakuleta jibu lolote la barua hii. Sasa mara nyingine tena Bwana Daktari ametaka kushuhudia ishara na kwa hisani yake ameondoa sharti lake la awali, na anataka ashuhudie ishara tu, iwe ishara yoyote, lakini iwe imezidi uwezo wa mwanadamu. Hivyo basi, tarehe hii ya leo, yaani 11 Januari 1892, siku ya Jumatatu Bwana Daktari Ametumiwa barua ya rejista kwa kumwita kwenye haki, ambayo madhumuni yake ni kwamba kama wewe upo tayari kusilimu kwa moyo wa kweli kwa kushuhudia ishara isiyo makhsusi, basi achapishe ikirari yake kwa kula kiapo katika magazeti yaliyotajwa chini ya ukurasa[36] kuwa mimi fulani bin fulani mkazi wa mji fulani katika Utawala wa Jammu ninafanya kazi ya udaktari, wakati huu kwa kuapa nafanya ikirari sahihi kwa nia njema na kwa kutafuta haki na kwa ikhlasi ya moyo kuwa kama nikishuhudia ishara yoyote ya kuisaidia Islam, ambayo nishindwe kuonyesha mfano wake na nisiweze kuonyesha mfano wake wowote katika nguvu za kibinadamu pamoja na

[36] Panjab Gazeti Sialkot, Jarida la Anjuman Himayate Islam Lahore, Nadhimul Hind Lahore, Akhbare Aam Lahore, Nur Afshan Ludhiana.

masharti yake yote, hapo mimi bila kusita nitasilimu. Maandishi haya na ikirari hii inahitajika kwa sababu Mwenyezi Mungu Mhifadhi wa milele na Mtakatifu Haonyeshi ishara kame mchezo. Maadamu mtu hamwelekei kwa unyenyekevu kamili na kwa shabaha ya kutafuta muongozo, Yeye Huwa Hamwelekei kwa mtazamo wa rehema. Na kwa kuchapisha maandishi, ikhlasi na nia imara huthibitika. Na kwa vile mimi baada ya kufahamishwa na Mwenyezi Mungu nimetangaza ahadi ya dhihirisho la ishara katika muda wa mwaka mmoja, hivyo muda huo huo utakuwa kwa ajili ya Bwana Daktari pia. Kwa mtafuta ukweli, huu sio muda mrefu. Kama mimi nikishindwa, basi adhabu na malipo yoyote Bwana Daktari atakayopendekeza sawa na uwezo wangu, mimi nitaikubali. Na Wallahi katika hali ya kushindwa niko tayari kukubali hata adhabu ya kifo.

ہماں بہ کہ جاں در رہِ او فشانم        جہاں راچہ نقصاں اگر من نمانم[37]

والسلام علی من اتبع الهدٰی[38]

Mtangazaji mwenezi.

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, Mungu Amsamehe 11 Januari 1892

---

**37** Tafsiri ya ubeti wa Kiajemi: Afadhali niitolee njia yake uhai wangu, kwani dunia itapata hasara gani nisipokuwepo. Mwenezi.

**38** Na amani iwe kwa aufuataye mwongozo. Mwenezi.

## Kwa Waadilifu Kuzingatia

Hili ni jambo la kweli kabisa kuwa macho ya moyo yanapofumbika, macho ya kimwili bali hisia zote za mwili pia hufumbika. Hapo mtu akiona haoni, na akisikia hasikii na akifahamu hafahamu, na ulimi hauwezi kunena ukweli. Hebu, angalieni kuwa masheikh wetu ingawa wanaitwa wenye akili, lakini kwa sababu ya chuki wamezama katika ujinga. Na mithili ya maadui wa kidini hatimaye wameanza kufanya uzushi. Mmoja wao ameandika kunihusu mimi kuwa alitoa habari ya mtoto wake mmoja kutokana na ufunuo kwamba atakuwa bingwa, ilhali yeye akafariki baada ya kuishi miezi michache tu. Nashangaa kwamba masheikh hao wenye haraka, kwa nini wakati wa kusema mambo kama hayo hawaikumbuki aya لَّعۡنَتَ اللّٰهِ عَلَى الۡكٰذِبِيۡنَ[39] , na kwa nini mara moja wameanza kuonyesha ukoma wao wa ndani na uadui dhidi ya Islam. Kama wana haya hata chembe, basi wathibitishe kuwa katika ufunuo wangu gani imeandikwa kuwa mwana aliyefariki kwa hakika yeye ndiye mwana wa ahadi? Katika ufunuo mna habari kwa jumla kuwa mvulana wa aina hii atazaliwa, na ufunuo Mtakatifu wa Allah haukuashiria kwenye mtoto fulani kuwa ndiye mwenye kutimiza bishara hii

---

[39] Laana ya Mungu iwe juu ya waongo" Aali 'Imraan, 3:62 Mwenezi.

kwa kumwashiria. Bali katika tangazo la mwezi Februari 1886 mna bishara kuwa baadhi ya wavulana watafariki pia utotoni. Basi, kwa kufariki kwa mtoto huyu imetimia bishara moja au imebatilika ishara fulani? Sasa, nasema kwa mfano kwamba kama kwa kufunya ijtihadi nimfikirie mwanangu yeyote kuwa labda yeye ndiye mwana aliyeahidiwa na fikara yetu ikosee, basi katika hali hii ufunuo utakuwa na kosa gani? Je katika ijtihadi za manabii hakuna mfano wake? Kama nimeandika ufunuo wazi katika kitabu changu chochote kuhusu mtoto aliyefariki basi uleteeni. Kusema uongo ni sawa na kula kinyesi. Inastaajabisha kuwa kwa nini watu hao wana shauku ya kula kinyesi, mpaka hivi leo mamia ya funuo zimedhihiri barabara ambazo zilitangazwa duniani lakini masheikh hao kwa 'kuihurumia' Islam hawakuitaja hata moja. Mamia ya watu waliambiwa mapema kuhusu Dilip Sing kushindwa kuja kuizuru India na Panjab. Baadhi ya mabaniani waliambiwa juu ya kifo cha Pandit Dayanand miezi michache kabla ya kufa kwake. Na mtoto huyu Bashiruddin Mahmud aliyezaliwa baada ya mvulana wa kwanza, habari ya kuzaliwa kwake ilitolewa katika tangazo moja kabla ya kuzaliwa kwake. Sardar Muhammad Hayat Khan aliposimamishwa kazi, wakati huo nikatoa taarifa kwa watu kuhusiana naye kuwa atarudishwa kazini.

Habari ya Bwana Sheikh Mehr Ali, tajiri wa Hoshiarpur kupatwa na janga ilielezwa kabla ya wakati, kisha habari ya kuachiliwa si tu alifikishiwa kabla ya wakati, bali mamia ya watu walitangaziwa hiyo. Kadhalika zipo ishara mamia kadha ambazo mashahidi waliozishuhudia wapo. Je, masheikh hao 'wanyofu' wamezizungumzia ishara hizo hata mara moja? Yule aliyepigwa muhuri na Mwenyezi Mungu moyoni mwake, nani aufungue moyo wao! Hata sasa pia watu hao wakumbuke kuwa uadui wao hauwezi kuidhuru Islam katu. Watajifia wenyewe kama wadudu, lakini nuru ya Uislamu itazidi kuendelea siku hadi siku. Mwenyezi Mungu Amependa kuieneza nuru ya Islam duniani. Baraka za Islam haziwezi kuzuilika kwa kelele za masheikh hawa wenye tabia ya nzi. Mwenyezi Mungu Ameniambia kwa maneno ya wazi kabisa:

أَنَا الفتّاح افتح لك۔ ترى نصرًا عجيباً و يَخِرّون على المساجد۔ ربنا اغفرلنا
انا كنا خاطئين۔ جلابيب الصدق۔ فاستقم كما امرت ۔ الخوارق تحت
منتهى صدق الاقدام ۔ كن لِلّٰه جميعًا و مع الله جمعيا ۔ عسٰى ان يبعثك ربّك
مقامًا محمودا

Yaani, Mimi ndiye Mshindishi, nitakupa ushindi, utaona msaada wa ajabu, na wakanao, yaani baadhi yao wenye bahati ya kuongoka wataangukia viungo vya  sijida wakisujudu huku wakisema Ee Mola wetu, tusamehe dhambi zetu, tulikuwa wakosaji. Haya ni

manufaa ya ukweli yatakayodhihirika. Basi, kama ulivyoagizwa, uwe imara. Mambo yasiyo ya kawaida, yaani karama zinadhihirika pale ambapo ndipo daraja ya juu kabisa ya ukweli. Uwe kwa Mungu kikamilifu, uwe pamoja na Mungu kikamilifu, huenda Mungu Akakuinua cheo kinachosifika. Na katika ufunuo mmoja kwa maneno yaliyorudiana na pengine kupishana kidogo akasema: Mimi Nitakupa heshima na Nitakukuza na nitatia baraka katika mabaki yako mpaka wafalme watatafuta baraka kutoka ndani ya nguo zako. Sasa enyi masheikh! Enyi wenye tabia ya ubahili! Kama mna nguvu, zizuieni bishara hizi za Mwenyezi Mungu zisitimie. Tumieni hila yenu ya kila namna na msiache hila yoyote, kisha muone kuwa Mkono wa Allah unashinda au mkono wenu?

والسّلام علیٰ من اتبع الھدٰی [40]

اَلْمُنَبِّہ النّاصح [41]

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian

**40** Na amani iwe kwa afuataye mwongozo. Mwenezi.

41 Mtanabahishaji, Mnasihi-

## Bwana Mir Abbasi Ali wa Ludhiana

چو بشنوی سخن اہل دل مگو کہ خطاست      سخن شناس نۂ دلبرا خطا اینجا است [42]

Huyu Bwana Mir ndiye yule ambaye nimeandika kumbukumbu yake nzuri katika uk. 790 wa Izaala Auhaam katika jumuiya ya waliofanya bai'ati. Ni masikitiko kuwa yeye ameteleza kwa kutiliwa wasiwasi moyani na baadhi ya watiao wasiwasi, bali ameshaungana na kundi la maadui. Baadhi ya watu watashangaa kuwa kumhusu yeye nilifunuliwa ufunuo kuwa اصلها ثابتٌ وفرعها فى السمآء[43]

Jibu lake ni hili kuwa maana ya ufunuo ni hii tu kuwa asili yake ni thabiti na tawi lake liko mbinguni, haikuelezwa kuwa kulingana na asili yake, yeye ni thabiti upande gani. Bila shaka jambo hili linapaswa kukubaliwa kuwa kila mtu huwa na sifa fulani ya kiasili ndani yake anayoshikilia kwa uthabiti na kwa kudumu. Na kama kafiri mmoja akiacha ukafiri ajiunge na Uislamu, yeye huja akiwa na sifa yake njema ya kiasili na kisha anapokwenda kutoka Islam kwenye ukafiri, basi hurudi tu na hiyo sifa yake. Kwani hakuna mabadiliko na mageuzi katika asili ya

---

42 Usikiapo maneno ya mja wa Mungu, usiseme hayo yana makosa. Mpedwa wangu, kosa lenyewe ni kwamba huna uwezo wa kutambua nukta. Mwenezi.

43 Mzizi wake ni imara na tawi lake lafika mbinguni. Mwenezi.

Allah na uumbaji wa Allah. Watu ni kama aina mbalimbali ya migodi. Mtu fulani ni kama mgodi wa dhahabu, mwingine kama mgodi wa fedha, mwingine kama mgodi wa shaba. Hivyo, kama katika ufunuo huo sifa fulani ya kiasili ya Bwana Mir imeelezwa ambayo haibadiliki basi si ajabu wala si jambo la kupinga. Bila shaka jambo hili linakubalika kuwa sio Waislamu tu bali makafiri pia wana baadhi ya sifa njema za kiasili na wanazo baadhi ya khulka kiasili. Mwenyezi Mungu Hakukiumba kitu chochote kikiwa giza tupu na katika kiza moja kwa moja. Naam, ni kweli kuwa uzuri wowote wa asili hauwezi kusababisha wokovu katika Akhera bila kupata njia iliyonyooka ambayo kwa maneno mengine inaitwa Islam. Kwani wema wa daraja ya juu ni imani, utambuzi wa Mungu, kufuata njia iliyonyooka na Uchamungu. Kama haya hayapo, basi sifa zingine zinakuwa si kitu. Isitoshe, ufunuo huu ni wa wakati ule ambapo Bwana Mir alikuwa imara, alikuwa na nguvu ya hali ya juu sana ya ikhlasi, na hata yeye pia alikuwa na dhana hii hii moyoni kuwa mimi nitakuwa imara vivyo hivyo. Hivyo, Mwenyezi Mungu Alitoa habari ya hali yake ya wakati huo. Jambo hili katika mafundisho ya ufunuo wa Mwenyezi Mungu linajulikana kwamba Yeye Hutoa habari kulingana na wakati uliopo, Anamwita tu kafiri yule anayekuwa

katika hali ya kufuru, na katika hali ya kuwa mwaminio na imara Humwita tu mwaminio mwenye ikhlasi na imara. Katika Neno la Mungu kuna mifano ya namna hii mingi sana, na hakuna shaka kuwa Bwana Mir kwa muda wa miaka kumi alikuwa miongoni mwa wafuasi wangu kwa uaminifu mkubwa, upendo na uimara. Na kwa jazba ya ikhlasi, wakati wa kufanya bai'ati si yeye peke yake tu bali aliwaingiza katika Jumuiya hii ndugu zake wengine, rafiki zake na jamaa zake pia. Na katika muda huo wa miaka kumi, barua alizoniandikia zilizojaa upendo na ikhlasi siwezi kuelezea hivi sasa makisio yake. Lakini, ninazo hata hivi sasa barua zake mia mbili ambamo kwa unyenyekevu wa hali ya juu alieleza ikhlasi na uaminifu wake. Bali, katika baadhi ya barua aliandika ndoto zake ambamo kana kwamba akasadikisha kiroho kuwa mimi nimetoka kwa Mungu, na kwamba wapinzani wangu wako upande wa batili. Na kwa sababu ya ndoto zake hizo anadhihirisha kuwa Yu pamoja nami daima, kana kwamba yu pamoja nami katika dunia hii na katika ulimwengu ujao. Na vivyo hivyo alizisambaza ndoto hizo katika watu na aliwaelezea wafuasi wake na waaminifu wake. Basi, ni dhahiri kuwa mtu aliyeonyesha uaminifu wake kwa jazba kiasi hiki, kuhusu hali ya wakati huo ya mtu kama huyu kama Mwenyezi Mungu Alete ufunuo

kuwa yeye wakati huu yu imara wala hatetereki, je ufunuo huu utachukuliwa kuwa ni kinyume cha hakika? Funuo nyingi zinaonyesha hali ya wakati uliopo tu, na hazihusiani na hali ya baadaye. Isitoshe, maadamu mtu bado yu hai, hukumu juu ya hatima yake mbaya haiwezi kukatwa, maana moyo wa mtu uko mikononi mwa Mungu Mwenye shani. Achilia mbali Bwana Mir, Yeye Akitaka, Anaweza kumleta mara moja kwenye haki yule mwenye moyo mgumu sana katika duina aliyepigwa muhuri juu ya moyo wake. Hivyo, basi, ufunuo huo ulihusiana na hali iliyokuwepo, si lazima ueleze habari za mwisho wake, na mwisho bado haujadhihirika. Wengi walitengana na wakweli na wakawa maadui wakubwa, lakini baadaye wakaona maajabu fulani, wakajuta na wakaangua kilio, wakakiri dhambi yao na wakarejea. Moyo wa mtu uko mkononi mwa Mwenyezi Mungu, na majaribio ya Yule Mwenye hekima yanamwandama mtu pamoja. Basi, Bwana Mir, kutokana na kasoro na mapungufu yake fulani yaliyofichikana amepata majaribio, na kisha kutokana na athari ya mtihani huo badala ya jazba ya upendo 'uyabisi' wa roho ukazuka uliosababisha 'ukavu' na ugeni, na ugeni ukazaa utovu wa adabu, na utovu wa adabu ukapiga muhuri moyoni, na muhuri wa moyo ukazaa uadui wa wazi na nia ya kudhalilisha na

dharau. Ni pahali pa kujifunza somo, maana alitokea wapi na amefikia wapi! Je kuna mtu aliyedhania kuwa hali ya Mir Abbas Ali itakuwa hivi. Mmiliki wa Ufalme hufanya Atakavyo. Marafiki zangu wanatakiwa wamuombee dua, na wasimnyime huruma zao ndugu yao mnyonge aliyetoka, nami pia, Mungu Akipenda, nitamuombea dua. Nilitaka ninakili humu katika kijitabu hiki baadhi ya barua zake kama mfano kuwadhihirishia watu kwamba ikhlasi ya Mir Abbasi Ali ilifikia daraja gani, na ndoto za aina gani alikuwa akidhihirishia daima, na kwa maneno gani ya aina gani ya unyenyekewu na maneno ya heshima kubwa alikuwa akiandika ndani ya barua zake. Lakini nasikitika kuwa ndani ya kijitabu hiki kidogo nafasi haimo. Mungu Akipenda sawa na haja barua hizo zitadhihirishwa katika wakati mwingine. Huu ni mfano mmoja wa mabadiliko ya mwanadamu, kwamba mtu yule ambaye juu ya moyo wake daima adhama na heba ya upendo wa kweli ulitawala na ambaye ndani ya barua zake alikuwa ananitaja kuwa khalifa wa Mungu ardhini, leo hali yake ikoje! Hivyo basi, Muogopeni Mwenyezi Mungu na daima ombeni kwamba kwa fadhili zake tu Aimarishe mioyo yenu kwenye haki na Akuepusheni na kuteleza. Msiutegemee uimara wenu. Je kuna mtu aliyempita Umar Faruk[ra] katika uimara ambaye alipatwa na

jaribio kwa kipindi kifupi tu. Na kama mkono wa Mwenyezi Mungu usingemkinga, basi Mungu Anajua hali ingekuwaje. Ingawa nimehuzunika sana kutokana na kuteleza kwa Mir Abas Ali, lakini naona kuwa maadamu mimi nimekuja nikiwa mfano wa Hadhrat Masihi[as], basi ililazimu pia kuwa katika matukio ya baadhi ya wafuasi wangu wanaodai ikhlasi, uonekana pia mfano huo. Jambo hili ni dhahiri kuwa baadhi ya marafiki mahususi wa Hadhrat Masihi[as] waliokuwa wanadani wake ambao katika kuelezea sifa zao ufunuo wa Mungu pia ulishuka, mwishoni waliachana na Hadhrat Masihi[as] . Yuda Iskariote alikuwa mwandani sana wa Hadhrat Masihi[as] aliyekuwa mara nyingi akila pamoja na Hadhrat Masih katika chombo kimoja na alikuwa akionyesha upendo wa hali ya juu sana, ambaye alipewa bishara ya kiti cha kumi na mbili cha peponi. Hata Bwana Petro alikuwa mfuasi mwema sana ambaye kumhusu yeye Hadhrat Masihi[as] alisema kuwa funguo za mbinguni zimo mkononi mwake, naye alikuwa na madaraka ya kumwingiza peponi yeyote amtakaye na kuacha kumuingiza amtakaye. Lakini mwishoni mambo aliyoyafanya Bwana huyu, wasomi wa Biblia wanatambua kuwa akisimama mbele ya Masihi[as] na kuashiria kwake akasema kwa sauti kubwa kuwa, Mungu Apishe mbali, mimi namlaani mtu huyu.

Bwana Mir bado hajafikia hatua hiyo. Nani anajua kitatokea nini kesho? Ingawa kuteleza huku kulikuwa katika bahati ya Bwana Mir, na kiwakilishi nomino cha kike katika أَصلها ثابتٌ pia kiliashiria kwenye hiyo, lakini uchochezi wa Sheikh Batalawii ulimfanya Bwana Mir azidi kuteleza. Bwana Mir ni mtu wa kawaida tu, masiala mengi ya dini yeye hayajui. Bwana Batatalwii na wengineo wakamhamakisha kwa vichocheo vya kuleta uchafuzi kwa kusema angalia, jambo fulani ni kinyume cha itikadi ya Islam, na neno fulani eti ni la utovu wa adabu. Nimesikia kuwa sheikh Batalawii amekwisha kula kiapo kuhusiana na wafuasi wangu wenye ikhlasi kwamba لَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِيْنَ[44]

Amepita kiasi hiki kwamba katika maneno yake hakuna kumwacha hata sheikh Najdi, ili angewatenga angalau watu wema. Ingawa kwa sababu ya baadhi ya wafuasi waliorudi nyuma yeye anafurahi sana, hata hivyo yeye anatakiwa aelewe kwamba kwa kunyauka tawi moja bustani yote haiwezi kuharibika. Tawi ambalo Mwenyezi Mungu Anataka, Hulikausha na kulikata, kisha Hutoa badala yake matawi mengine yaliyojaa maua na matunda kochokocho. Sheikh Batalawii akumbuke kuwa mtu mmoja akitoka ndani ya Jumuiya hii, Mwenyezi Mungu Atawaleta ishirini

---

[44] Hakika nitawapoteza wote. Mwenezi.

badala yake. Azingatie sana aya hii:

فَسَوۡفَ یَاۡتِی اللّٰہُ بِقَوۡمٍ یُّحِبُّہُمۡ وَ یُحِبُّوۡنَہٗۤ ۙ اَذِلَّۃٍ عَلَی الۡمُؤۡمِنِیۡنَ اَعِزَّۃٍ عَلَی الۡکٰفِرِیۡنَ [45]

Mwishoni, tunawadhihirishia wasomaji kuwa Bwana Mir Abbas Ali alitoa kipeperushi tarehe 12 Desemba 1891 cha upinzani kilichojaa maneno yenye utovu wa adabu na ya dharau. Hatujihusishi hata kidogo na maneno yake. Moyo unapochafuka, basi na ulimi pia unachafuka papo hapo. Lakini yalazimu mambo matatu ya kipeperushi hiki yajibiwe:

Mosi: Hali ya mijadala ya Delhi imegandama moyoni mwa Bwana Mir kinyume cha tukio lenyewe. Basi, tangazo langu hili linatosha kuondoa wasiwasi huo, sharti Bwana Mir alisome kwa makini.

Pili: Ndani ya moyo wa Bwana Mir, imeimarika, kimakosa kabisa, ya kuwa mimi ni mtu nisiyemsadiki Mungu, naikana miujiza na kuikataa Lailatul Kadri, nadai kuwa nabii, nawafedhehesha manabii na ninazikana itikadi za Islam. Hivyo kuondoa wasiwasi huu, mimi nimekwisha ahidi kwamba kijitabu peke yake kitatolewa hivi karibuni kutoka kwangu. Kama Bwana Mir akisoma kijitabu hicho kwa makini, atajutia sana dhana zake mbaya zisizo na msingi na

[45] Basi, kwa yakini Mungu Ataleta watu ambao Atawapenda nao watampenda, wapole kwa waaminio, wakali kwa makafiri. Al-Maaida, 5:55. Mwenezi.

uhakika wowote, sharti ajaliwe na Mungu.

Ya tatu ni kwamba katika kipeperushi chake hicho, Bwana Mir akieleza karama zake akaandika kana kwamba ana uwezo wa kuonyesha Mtume[saw]. Hivyo, katika kipeperushi hicho anaandika kuhusiana nami kuwa hakushindana nami katika jambo hili. Mimi nilisema kuwa sisi wawili tukae katika msikiti wowote na kisha ama nifanywe kuonana na Mtume[saw] ambaye asadikishe madai yako, au mimi nikufanye uonane na Mtume[saw] ambaye atoe uamuzi kuhusu jambo hili. Maandishi haya ya Bwana Mir hayakunistaajabisha mimi tu, bali kila anayeelewa habari hii anastaajabu sana kuwa kama Bwana Mir alikuwa na uwezo na sifa ya kumuona Mtume[saw] wakati wowote apendapo na kumuuliza mambo, bali awaonyeshe wengine pia, basi kwa nini alifanya bai'ati kwangu bila kusadikishiwa na Mtume[saw]? Na kwa nini akaendelea kuwepo ndani ya kundi la wenye kuonyesha ikhlasi kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo? Ajabu ni kwamba hata mara moja Mtume[saw] hakumtokea ndani ya ndoto kumwambia kuwa kwa nini unafanya bai'ati kwa mwongo na mdanganyifu huyu asiye na dini? Na kwa nini unajinasa katika upotofu. Je mtu yeyote mwenye akili anaweza kuelewa kuwa mtu mwenye uwezo na madaraka ya kumtembelea Mtume[saw] mara kwa mara

na kutekeleza maagizo yake, na kushauriana naye, yeye mtu huyo kwa muda wa miaka kumi mfululizo awe amenaswa na mwongo na mdanganyifu, na awe mfuasi wa mtu aliye adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume na anayemdharau Mtume[saw], na ni mwenye kuanguka chini kabisa. Jambo la kustaajabisha zaidi ni hili kuwa baadhi ya marafiki wa Bwana Mir wanasema kuwa yeye aliwasimulia baadhi ya ndoto zake, akawaambia kuwa yeye alimuona Mtume[saw] ndani ya ndoto, na Mtume[saw] akamwambia kunihusu mimi kuwa kwa kweli mtu huyo ni Khalifa wa Allah na ni Mujadidi wa dini. Na barua kadha za madhumuni haya Bwana Mir aliniandikia mimi pia ambamo ndoto za aina hii zimeelezwa na kusadikisha madai yangu. Sasa mtu muadilifu anaweza kuelewa kuwa kama Bwana Mir anaweza kumuona Mtume[saw] ndani ya ndoto, bila shaka aliyoyaona kwanza yapasa kukubaliwa. Na endapo ndoto zake hizo hazifai kuaminika na ni ndoto zilizovurugika, ndoto kama hizo hata siku za baadaye pia haziwezi kuaminika. Wasomaji wanaweza kufahamu kuwa dai la kuwa na uwezo wa kumwonesha Mtume kwa wengine ni upuuzi mkubwa namna gani. Ni dhahiri kutokana na Hadithi sahihi kuwa ndoto ile tu ambamo mtu anamwona Mtume[saw] yaweza kuepukana na mwigo

wa Shetani ambamo Mtume[saw] ameonekana kwa umbo na sura yake, waila shetani kuiga sura za manabii si tu kunajuzu bali kwa kitendo kwatokea hasa. Shetani mlaaniwa anaonyesha hata mwigo wa Mungu na kudhihirisha mng'ao wa Arshi, basi ana shida gani kuiga sura ya Manabii! Sasa kama hali ndiyo hii, basi hata tukikubali, kwa mfano kuwa mtu fulani amemwona Mtume[saw] ndotoni, twawezaje kutulia kwamba yeye kweli amepata kumwona Mtume[saw], maana watu wa zama hizi hawajui sura hasa ya Mtume[saw], na ni jaizi shetani kujionyesha katika sura ghairi yake. Hivyo basi, kwa watu wa zama hizi alama ya kweli ya kumuona kwelikweli ni hii kwamba pamoja na kuona baadhi ya miujiza na alama mahususi pia zipatikane ambazo kwazo iyakinike kwamba ruiya au kashfi hii imetoka kwa Mungu. Kwa mfano, Mtume[saw] aeleze baadhi ya bishara kabla ya kutokea kwazo, au atujulishe kabla ya kutukia baadhi ya mambo ya ushukaji wa kudra, au atujulishe mapema kukubaliwa kwa baadhi ya maombi, au atuambie maelezo ya kina na maarifa ya aya za Kurani Tukufu ambayo hayajapata kuandikwa wala hayajachapishwa hapo kabla, hapo bila shaka ndoto ya aina hii itaonekana kuwa sahihi. Waila mtu mmoja akidai kuwa Mtume[saw] alinijia ndani ya ndoto na

kasema kuwa mtu fulani bila shaka ni kafiri na dajali, sasa nani aamue kuwa hii ni kauli ya Mtume[saw] au ni kauli ya shetani au yule mwotaji ameizua yeye mwenyewe kwa ujanja? Hivyo, kama kwa kweli Bwana Mir ana uwezo huu kuwa Mtume[saw] anamjia ndotoni mwake, sisi hatutaki kumsumbua Bwana Mir kwamba lazima atuonyeshe, bali yeye athibitishe kumwona mwenyewe tu, na kwa njia ya alama hizo nne zilizotajwa hapo nyuma athibitishe kwamba kwa kweli yeye amemuona Mtume[saw], nasi tutakubali. Na endapo yeye ana shauku tu ya kushindana, hapo atumie njia sahihi ya mashindano tuliyoieleza ndani ya tangazo hili. Sisi kwa hakika tunayo shaka katika kumuona kwake Mtume[saw], achilia mbali kukubali kwamba anaweza kuwaonyesha wengine Mtume. Hatua ya kwanza ya mtihani ni hii kwamba je Bwana Mir yu mkweli katika dai lake la kumwona Mtume au yu mwongo? Kama yu mkweli, basi atangaze ndoto au kashfi yake yoyote ambamo iwe imeelezwa kuwa amemwona Mtume[saw], na yeye alieleza kama alama ya kuzuru kwake bishara fulani fulani na kupokelewa dua na kudhihirisha mambo ya kweli na maarifa, kisha baadaye atoe mwito wa kumwonyesha Mtume kwa wengine. Nami kwa kutilia nguvu ukweli niko tayari kwa jambo hili pia kwamba Bwana Mir

aonyeshe ajabu la kumwonesha Mtume pia. Yeye aje Qadian, msikiti upo, gharama zake zote za kwenda na kurudi pamoja na chakula zitakuwa juu yangu. Nami nawaambia wasomaji wote kuwa haya ni majivuno tu matupu na kamwe hawezi kuonyesha chochote. Kama akija, atafedheheka tu. Wenye akili wanaweza kufikiria kuwa mtu aliyefanya bai'at, akaingia katika kundi la wafuasi na kwa muda wa miaka kumi akaendelea kunitambua mimi kuwa Khalifa wa Mungu, Imamu na Mujadidi, na akaendelea kunielezea ndoto zake, je yu mkweli katika dai lake hili? Hali ya Bwana Mir ni ya kusikitisha sana, Mungu Amrehemu! zisubirini bishara zitakazodhihiri. Angalieni ukurasa 855 wa Izaala Auhaam. Zisome kwa makini kurasa wa 635 na 396 za Izaala Auhaam. Isubirini bishara ya tangazo la 10 Julai 1887 ambalo pamoja nalo kuna ufunuo huu pia:

ویسئلونك أَحق هو قل ای وربی انه لحق وما انتم بمعجزین۔ زوجنا کها لا
مبدل لکلماتی۔ وان یروا اٰیة یعرضوا ویقولوا سحر مستمر

Na wanakuuliza, je jambo hili ni kweli? Sema, ndiyo, haki ya Mola wangu ni kweli, na nyinyi hamwezi kulizuia jambo hili kutokea. Sisi Wenyewe Tumekufungisha ndoa naye. Hakuna anayeweza kubadilisha maneno yangu. Watageuza uso baada ya kuiona ishara na hawataikubali, na watasema kuwa

huu ndio udanganyifu au uchawi halisi.

28-27-14-2-27-2-26-2-28-1-23-15-11-

1-2-27-14-10-1-38-27-47-16-11-34-14-11

7-1-5-34-23-34-11-14-7-23-14-1-1



14-5-28-7-34-1-7-34-11-16-1-14-7-2-1-7-5-1-14-1-

14-2-28-1-7-

والسلام علی من فهم اسرارنا و اتبع الهدی[46]

Mtoaji nasaha mwenye huruma, Ndimi
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,

27 Desemba 1891

[46] Na amani iwe kwa azifahamuye siri zetu na afuataye mwongozo. Mwenezi.

## Taarifa

Ndugu wote wenye ikhlasi waliofanya bai'ati yangu wajue kuwa shabaha ya kufanya bai'ati ni kwamba mapenzi ya dunia yapoe, na mapenzi ya Mola Mtukufu na ya Mtume Mtukufu[saw] yatawale moyoni. Na hali ile ya kutengana na dunia ipatikane ambayo kwayo safari ya Akhera isionekane yenye kuchukiza. Lakini kwa kulipata lengo hili yamlazimu mtu kukaa nami na kutumia muda fulani wa umri wake katika njia hii ili, Mungu Akipenda, kwa kushuhudia dalili yenye yakini, udhaifu na uzembe uondoke, na kwa kuzalika yakini kamili izalike shauku na ladha ya jazba ya upendo mkubwa. Hivyo, kwa ajili ya jambo hili daima inatakiwa kuwa na hadhari na yapasa kuomba dua kuwa Mungu Ajaalie uwezo huu. Na mpaka uwezo huo haujapatikana inapasa kuonana nami mara kwa mara, kwani baada ya kuingia katika silsila ya baiati, kisha kutojali kuonana, baiat kama hii haina baraka, itakuwa ni kama kufuata mazoea. Na kwa vile ni vigumu kwa kila mmoja kuja hapa akae nami kutokana na udhaifu wa asili au upungufu wa uwezo au kitalifa kirefu, au kuja mara chache kwa mwaka kuonana nami kwa kuvumilia shida kubwa, kwani hivi sasa ndani ya mioyo mingi hamna shauku nyingi kiasi kwamba waweze kuvumilia taabu kubwa na madhara mengi, kwa hiyo inaonekana inafaa

zipangwe siku tatu kwa mwaka kwa ajili ya mkutano ambamo, Mungu Akipenda, ndugu wote waaminio waweze kuhudhuria katika tarehe zilizopangwa, sharti wakiwa na afya na nafasi na kutokuwa na vikwazo vikubwa. Kwa maoni yangu ni bora tarehe hizo ziwe 27, 28 na 29 za mwezi Desemba. Yaani baada ya siku ya leo hii iliyo 30 Desemba 1891, kama tarehe 27 Desemba ikifika katika uhai wetu, basi ndugu wote kadri ya wasaa wao wanapaswa wafike kwenye tarehe hiyo kwa ajili ya kusikiliza maneno ya Mwenyezi Mungu tu na kwa ajili ya kushiriki katika maombi. Na Katika mkutano huo kutakuwa na shughuli za kuelezea mambo ya ukweli na maarifa ambayo ni ya lazima kwa ajili ya kuzidisha imani na yakini na maarifa. Na vile vile kwa jamaa hao kutafanyiwa maombi maalum na mwelekeo mahususi na itafanyawa bidii sawa na uwezo mbele ya Mungu Mrehemevu kwamba Mwenyezi Mungu Awavutie kwake na Awakubalie kwake na Awapatie mabadiliko mema. Na faida nyingine ya muda itakayopatikana ndani ya mikutano hii ni kwamba kila mwaka ndugu wote wapya watakaoingia ndani ya Jumuiya, kwa kuhudhuria katika tarehe zilizopangwa wataweza kuonana na ndugu zao waliowatangulia, na kwa kujuana uhusiano wa upendo na udugu utaendelea kuzidi baina yao. Na ndugu atakayekuwa amefariki

dunia hii, ataombewa dua ya maghufira katika mkutano huo. Na kwa kuwafanya ndugu wote wawe kitu kimoja kiroho na kwa kuondolea ukavu wa tabia, ugeni na unafiki baina yao itafanywa juhudi katika Baraza la Mungu Mtukufu Mwenye shani. Na katika mkutano huo zitapatikana pia faida nyingine nyingi za kiroho na manufaa ambayo, Mungu Akipenda, yataendelea kudhihirika siku hadi siku. Na itafaa kwa watu wenye uwezo mdogo kuwa waanze mapema kufikiria njia ya kushiriki katika mkutano huo. Na kama kwa ajili ya gharama za safari ya mkutano huu ndugu waanze kujiwekea pesa kidogo kidogo pembeni kila siku au kila mwezi, bila shida pesa kwa ajili ya safari itapatikana, kana kwamba safari hii itakuwa bure. Na itakuwa vizuri kwamba miongoni mwa wenzetu, wale ndugu ambao wanaafiki mpango huu waniarifu sasa hivi kwa maandishi yao mahususi ili majina ya ndugu hao wote yahifadhiwe katika orodha moja kwamba wakijaaliwa nguvu na uwezo waahidi kuhudhuria kwenye tarehe maalum katika maisha yao yote, na wahudhurie kwa moyo wote na azma imara, isipokuwa vikitokea vikwazo vitakavyoifanya safari iwe nje ya uwezo wao. Na leo, tarehe 27 Desemba 1891, mkutano uliofanyika kwa mashauriano ya kidni, ndugu wote waliohudhuria kwa kuvumilia shida za safari kwa ajili ya Mungu tu, Mwenyezi

Mungu Awalipe malipo mema na Awajaalie thawabu ya kila hatua waliyochukua. Amin, thumma Amin.

## Tangazo

Tunazo nakala kadhaa za vijitabu Fa'the Islam na Taudhihe Maraam ambavyo bei yake ni Rupia moja, na zipo nakala kadhaa za kitabu Izaala Auhaam ambazo bei ya kila nakala ni Rupia tatu, gharama ya posta ni mbali na bei. Ndugu wanaotaka kununua waagize. Anwani ni hii: Qadian wilaya ya Gurdaspur, kwa mwandishi wa kijitaju hiki, au wakitaka wanaweza kuchukua toka Patiala kutoka kwa Bwana Mir Nasir Nawwab, mchoraji wa ramani, ofisi ya idara ya mto. Na vilevile vitabu hivi vimo katika Panjab Press Sialkot, kwa Bwana Maulawii Ghulam Qadir Fasihi mwenye kiwanda cha uchapishaji, mwaweza kuagiza kutoka huko pia.